# *Mng'ang'anizi*

Asanteni. Basi tunainamisha vichwa vyetu sasa kwa ajili ya maombi.

Baba yetu wa Mbinguni, tunashukuru kwa ajili ya hii, nafasi nyingine yenye neema sana ya kuiletea Chicago Injili ya Yesu Kristo, kwa hawa wateule wanaokungojea Kuja kwa Kristo mwenye haki. Tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba tutakapoondoka usiku wa leo, kwamba mioyo yetu na iwe kama ya wale waliokuwa wakitoka Emau, kasema, "Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu wakati Yeye aliposema nasi njiani?"

2 Tunakutarajia Wewe uje hivi karibuni, Bwana, kutupokea katika Ufalme Wako mkuu ng'ambo ya hapa, ambamo hakuna huzuni tena wala mauti, ambako hakutakuwa na mikutano mingine mirefu ya maombi tena, wala hakuna kuomba tena sana na watu, na yote yatakuwa yamekwisha wakati huo. Nasi tutaingia katika furaha za Bwana, ambayo sisi, kwa neema ya Mungu, tunajisikia kwamba sisi ni washiriki wake, kwa njia ya Yesu Kristo. Yajalie mambo haya, Baba.

3 Na kukiwako na mbegu yoyote ambayo imekuwa mioyoni mwa watu, na haijapata Uzima bado, jalia jambo fulani litendeke, usiku wa leo, ambalo litauhuisha Uzima huo, Bwana, kwa ufahamu wa Ujumbe wa wakati huu wa mwisho ambamo tunaishi.

4 Wabariki wahudumu hapa Chicago. Wabariki wafanyabiashara, Baba. Na kiamshakinywa cha kesho asubuhi, Ee Mungu, nipe kitu cha kusema ambacho kitawachochea hao watu, mioyo yao. Tujalie, Baba. Tusaidie basi, kesho usiku, huko Lane Tech. Na Jumapili, ibada mbili, kurudi hapa. Tujalie, Bwana. Jalia nafsi ziokolewe, watu waponywe, Ufalme wa Mungu uinuliwe, Bwana. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

Ketini.

5 (Mna ule wimbo kwa ajili ya asubuhi? Mna ule wimbo kwa ajili ya asubuhi?)

6 Nilifurahi nilipokuwa nikizungumza na Ndugu Vayle hapa dakika chache tu zilizopita. Niliingia kuchelewa kidogo tu, mimi mwenyewe.

7 Na ninajua kuna joto. Bali jiwazie tu umeketi hapo, halafu kutembea hapa juu, unaona. Na, bali daima sisi tuna furaha, haidhuri ni hali gani iliyopo, kuwa hapa. Wazieni tu juu ya siku za Bwana wetu, huko chini Palestina, wakati hiyo miale ya jua, joto, na koo Lake bichi, Yeye amesimama pale, na mnyonge sana na—na kuendelea kuhubiri, na kuwaponya wagonjwa. Yeye ni

yule yule leo tu kama alivyokuwa wakati huo. Angali anahisi vile vile. Hii, neema Yake imetosha kwa yote tunayohitaji.

8 Sasa, huu ndio usiku ambao mimi hujaribu kuziweka siku hizi tatu usiku kwa ajili ya kuwaombea wagonjwa na kuzungumza juu ya wagonjwa, maombi kwa ajili ya wagonjwa. Sasa, nyakati hizo zingine, nitazungumza vinginevyo, juu ya wokovu. Kwa sababu, nina ibada maradufu kila siku, mnaona, na siwezi, siwezi kuifanya. . . Kama nikihubiri kwa nguvu, inanibidi kula. Na kama nikila, siwezi kufanya ibada za namna hii, mnaona. Nami sina budi kuninii. . . wala siwezi kuwa na ibada mbili siku moja, na kuifanya moja ya hizo kuwa ibada ya uponyaji. Ni kwamba tu u—umejaa chakula, na damu yako imeenda tumboni mwako, kusaga chakula, na halafu akili yako haifanyi kazi vizuri, kwa njia hiyo.

9 Kwa hiyo ni—ningeninii, labda, pengine basi, niliwazia usiku wa leo tungeutoa kwa ajili ya kuwaombea wagonjwa, tena usiku wa leo. Nilimwambia Billy. Nafikiri alisema ya kwamba yeye. . . Je! alisambaza kadi za maombi, kuna yeyote ajuaye? [Kusanyiko linasema, "Ndiyo."—Mh.] Sawa. Sawa, basi, tutazifikia upesi tu tuwezavyo. Basi sasa hebu tuwe tu na kicho, tusikilize kwa makini. Na halafu katika mstari wa maombi, hebu tuje kwa heshima yote tujuayo jinsi, kuamini Mungu yupo hapa kutuponya.

10 Sasa tunashukuru sana kwa ajili ya maono. Hiyo ndiyo huduma yangu, imelenga hapo, kufikia karibu wakati huu; nikingojea dakika yoyote kitu kingine kije, ambacho kinakuja. Sasa nina kile ambacho kilinidhoofisha kidogo, ilikuwa ni juma hili lililopita.

11 Tulikuja nyumbani kutoka Arizona, na tunarudi moja kwa moja Jumatatu, huko Arizona. Halafu basi, nyumbani, nimekuwa na watu ambao wamekuwa wakingojea katika mstari huo kwa muda wa miaka mitatu au minne, kwa ajili ya usaili wa faragha, kutoka Texas, kutoka Arkansas, na kote nchini, wakingojea huo usa- wa binafsi. . . Hapo ndipo unapopata kitu halisi. Unapata, una mtu mmoja tu na wewe mmeketi pamoja, ndipo Roho Mtakatifu anaendelea tu kutenda kazi na kufunua.

12 Jambo dogo la kigeni lilitukia hivi majuzi. Nilikuwa na yapata kumi na watano, nadhani, ama ishirini, katika siku moja. Na nikiketi katika chumba changu cha kusomea, mapema asubuhi hiyo, kabla ya kwenda kule, Roho Mtakatifu mkuu aliingia na kuniambia kila mtu aliyekuwa anakuja, kila swali wangeliuliza, kila ndoto, na kila tafsiri. Nikayaandika kwenye karatasi, kisha nikaweka kila moja chini. Ndipo ningeingia chumbani, nao hawa watu, kamwe hatukuwa tumekutana hapo kabla. Angeingia na kuzungumza nao, na kuonyesha kila swali walilokuwa wameuliza na yote kulihusu, kwa utaratibu, na ndoto waliyokuwa nayo. Ndipo ninanyosha mkono na kukitwaa

kipande cha karatasi, na kuwakabidhi, ambapo ilikuwa tayari imesemwa kabla hata hawajafika kule, kile kingetukia.

13 Sasa, Mungu pekee ndiye anayeweza kufanya hilo. Mnajua nisingeweza kufanya hilo. Mtu yeyote anajua hiyo ni. . . kwamba—kwamba mwanadamu hawezi kufanya hilo. Hatuna njia ya kulifanya. Hicho ni kitendawili kingine, kama tulivyozungumzia jana usiku. Na halafu kuona usahihi wa Roho Mtakatifu, wakati anaposema jambo fulani litatukia, ni vivyo hivyo hasa.

14 Sasa kama yeyote wenu amesikia juu ya ono hilo la kwenda huko juu kwenye misitu ya kaskazini, kufikia mahali ambapo kamwe sikupajua, na kuhusu yule dubu wa futi saba, mwenye ncha za fedha, na yule kuro wa nchi arobaini na mbili, na mahali angekuwa amelala. Amelazwa sakafuni mwa chumba changu cha faragha, vivyo hivyo hasa. Ambapo ilisemwa, mahali paliposemwa, jinsi lingetukia, na neno kwa neno hasa.

15 Ni wangapi wamewahi kusikia ile kanda, *Mabwana, Ni Wakati Gani?* kabla tu sijaelekea Magharibi? Sababu ya Malaika wa Bwana kunituma huko nje, Yeye aliniambia, kasema, "Sasa, kutoka Mbinguni watakuja Malaika saba katika kundi, kutakuwa na watatu kila upande, na mmoja juu. Itakuwa kama pembetatu, ama kitu kama piramidi."

16 Nami nikasema, "Yule aliyekuwa upande wa kulia alikuwa amezirudisha mbawa Zake nyuma, nami nikaingia upesi katika kundi hilo, karibu na Yeye, na Yeye alikuwa aniambie la kufanya."

17 Ndipo nikaenda Magharibi, kama tu Yeye alivyoniambia, nilikuwa huko juu siku hiyo hiyo. Ndipo wakati walipoanza kushuka kutoka Mbinguni, nilisema, "Kutatokea sauti kama mlipuko mkuu, kitu kama ki—kikata cha ndege, kikata sauti kikitokea, lakini," nikasema, "itakuwa na sauti kubwa zaidi ya hiyo. Nami nitakuwa tu kaskazini-mashariki mwa Tucson, yapata maili hamsini ama mia moja, kitu kama hicho, nayo Tucson itakuwa imekaa *hivi*. Nami nitakuwa nikitoa namna fulani ya vichoma-nguo, ama vichwambuzi, ndivyo wanavyoviita kule, kutoka kwenye mguu wa suruali yangu." Kisha nikasema, "Mlipuko utatokea." Nasi tulikuwa kule juu siku hiyo, nami nilikuwa peke yangu. Kuna mtu, nafikiri Ndugu Sothmann yupo hapa usiku wa leo, aliyekuwa pamoja nami, yeye na Ndugu Norman.

18 Uko hapa, Ndugu Fred? Nilifikiri nilikusikia ukisema, "amina," hivi majuzi usiku. Nilifikiri alikuwa hapa; labda nilikosea. Mimi. . . Loo, samahani. Loo, naam, samahani, Ndugu Fred. Naam, tulikuwa kule juu.

19 Na kwenye siku hiyo kabla tu halijatukia, Roho Mtakatifu alikuja moja kwa moja kwenye maskini kambi tulimokuwa tumepiga kambi, na kusema, akaanza kufunua habari za watoto

wetu, na yale wanayopaswa kufanya, na jinsi ambavyo, kwamba ni hali gani, na mambo yaliyokuwa yakitukia miongoni mwao, na kutwambia la kufanya, na kadhalika. Ilinibidi tu niamke na kuondoka.

20 Na keshoye asubuhi. Nilikuwa nimepata mahali wale nguruwe mwitu walikuwa, na nilikuwa nikijaribu kuwaambia ndugu hawa wawili jinsi ya kuwafikia. Ndipo nikavuka mlima, nikashuka ninii kidogo, kile ambacho tungekiita, maskini kitu kama, mgongo wa nguruwe. Nami nilimfanya Ndugu Sothmann kuenda mahali pengine ambapo nilikuwa nimewaona hao nguruwe mwitu siku iliyotangulia. Nilikuwa tayari nimempata wangu, na kwa hiyo nilikuwa nikijaribu kuwaweka ndugu hawa mahali panapofaa kwa ajili yake.

Maana, ndugu hawa, mara nyingi mi—mimi huwaongozea.

21 Kisha nikamwambia Ndugu Norman aje upande huo mwingine, na kumweka Ndugu Fred katikati, halafu ningeenda *hivi*. Nami kama ningekimbia mlimani, nao wakimbie upande *huu*, ningepiga tu risasi hewani, kuwarudisha upande ule tena, kusudi apate kuchagua aliyemtaka.

22 Basi tukafika huko nje, na hapakuwapo na nguruwe mwitu. Nikamwangalia Ndugu Fred kwa darubini, yapata umbali wa maili moja, na ningeweza kumwona. Akarudi juu ya mlima, wakati nguruwe mwitu walipokosekana. Nikashuka chini ya mlima, kwenye shimo kubwa, nikapanda juu, nikaketi chini.

23 Ilikuwa yapata saa mbili asubuhi. Nami nilikuwa nimekunja miguu yangu. Na nilikuwa, kutoka kwa ovaroli yangu, nilikuwa nikitoa baadhi ya hivyo vichwambuzi. Ndipo nikasema, "Mwajua, angalieni hapa, si ni ajabu hiyo!" Nikasema, "Hii ni vile vile hasa, na mimi niko mahali pale kikamilifu, kaskazini-mashariki mwa Tucson, na Flagstaff, mnaona, na nitakuwa mashariki mwa flagstaff, kaskazini-mashariki mwa Tucson." Nami nikasema, "Hivi hapa vile vichwambuzi nilivyosema nitakuwa nikitoa kutoka kwenye suruali yangu." Nikasema, "Ajabu hiyo," nami nikakitupa tu chini, namna *hiyo*.

24 Ndipo nikaangalia juu, upande mmoja ng'ambo ya lile shimo kubwa, na kulikuwako na kundi zima pale juu. Walikuwa karibu katika umbali wa kupiga risasi. Kwa hiyo, ni—nisingewapiga risasi mimi mwenyewe, maana sikuwahitaji. Nikasema, "Laiti ningaliweza tu kumfikia Ndugu Fred na hao wengine, sasa, na kuwapeleka kule." Ndipo nikakimbia nikavuka genge dogo, na kupitia kwa mwamba majini. Basi nilipokuwa nikikimbia kule, mara ikasikika kana kwamba nchi nzima imetenganika, kwa mlipuko mkubwa hivyo. Nalo likanishtusha mpaka nikawazia. . .Nilikuwa nimevaa kofia nyeusi, kofia kubwa nyeusi, na hiyo inaonekana tu kama nguruwe mwitu hata hivyo, niliwazia mtu fulani alikuwa amenipiga risasi. Na—nayo ilinishtusha hata nikaruka juu hewani.

Mara tu nikawazia, "Kwani haya yote yanahusu nini?"

25 Niliona miamba ikiporomoka ubavuni mwa kilima, ikibingirika chini. Ndipo nikaangalia juu, kulikuwako na ile Duara nyeupe juu yangu pale, ikizunguka-zunguka. Hawa hapa wakaja Malaika saba, wakaja wakishuka chini kutoka hewani, wakanichukua juu, na kusema, "Rudi nyumbani kwako, Mashariki, mara moja, ukailete hiyo Mihuri Saba. Kwa kuwa, kuna siri saba, kwa kuwa Neno kamilifu limefunuliwa sasa katika siri hizi saba."

26 Kama hujawahi kusikia, kama uliwahi kuamini nilipata kusema chochote katika mahubiri, kilichovuviwa, hebu chukua hizo kanda za ile *Mihuri Saba*. Mimi si mwuza kanda. Mimi... Bw. Sothmann hapa huuza kanda, yeye na Bw. Maguire, bali mimi siuzi kanda. Wanazichukua. Na kama uliwahi kusikia chochote ambacho kweli, vile ninaweza kusema ni BWANA ASEMA HIVI, zipate hizo.

27 Na unajua, sio katika wakati huo, sikujua hilo; bali kamera kutoka kote nchini zilikuwa zikipiga picha ya Hilo, hapo Wingu jeupe lilipotulia, likaingia kwenye Associated Press. Ninafikiri gazeti lenu la Chicago lililitangaza, kila mahali. Jarida la *Life* lililichapisha. Ni wangapi wameliona mle, ambapo Bw.... Hilo, mnaona, hilo lilikuwa ndilo moja kwa moja pale, jinsi tu hasa ilivyosema, nikisimama moja kwa moja chini Yake wakati Hilo liliposhuka chini na kuumbika. Wakasema, "Lilikuwa mbali sana, na ni... wakachunguza nchini, hapakuwapo na ndege wala chochote mle ndani. Na lilikuwa juu kupita kiasi, maili ishirini na sita kwenda juu, ambapo hapana unyevu wala chochote. Usingeweza, wasingeweza kutoa unyevu, hata hivyo. Na maili thelathini toka upande Wake mmoja hadi mwingine."

28 Nalo Hili hapa likaja, likitulia. Basi angalia upande wa mkono wa kulia wa kundi hilo, kama si... Someni hizo kanda, ama sikilizeni ile kanda, *Mabwana, Ni Wakati Gani?* yapata miezi mitatu ama minne kabla halijatukia. Hilo hapo.

29 Hata sayansi haina budi kutambua Hilo kwamba ni kweli. Wanalichunguza Hilo. Wanasema ni siri wasiyoweza kufahamu. Sayansi huko chini Tucson wanajaribu kulielewa Hilo, kwamba Hilo ni kitu gani. Nilifikiri kwanza ningeenda kuzungumza nao; nikawaza, "La, ingekuwa tu ni kama ile picha ya Malaika wa Bwana kwenye ile picha, wasingeliamini Hilo. Hakuna haja ya kuwaambia." Kwa hiyo, bali unaona, mbele ya haya yote, inawapasa kujua kwamba ni Kweli, haidhuru, kwamba ni Kweli.

30 Ndugu, dada, sijui ni lini. Nitafanya safari yangu ya mwisho kuja Chicago siku moja. Huenda ikawa hii ndiyo. Bali ninawaambieni, katika Jina la Bwana Yesu, Injili ni ya kweli. Hizi ni siku za mwisho. Tunaishi katika vivuli vya Kuja Kwake. Lolote ufanyalo, fanya bidii kuingia katika Ufalme wa Mungu. Kama kuna mguso mmoja mdogo unaougusa moyo

wako, wewe njoo upesi wakati ukiwa na nafasi ya kuja. Maana, saa inakaribia ambapo itakuwa imechelewa kupita kiasi, na ndipo hutataka kuja tena, hakutakuwako na wito mwingine tena moyoni mwako. Halafu basi, haijalishi ulijaribu kiasi gani, kamwe hutaingia. Wakati mshirika wa mwisho akiongezwa kwenye Mwili huo, kwa ajili ya Unyakuo, kamwe hakutakuwako na mwingine atakayeokolewa; milango imefungwa, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, na hakutakuwa na wokovu mwingine utakaosalia, ingawa watu watadhani wataokoka, hapo ndipo shida itakapokuja. Mnaona?

31 Wakati mmoja Yesu alikuja, wanafunzi wa Yohana walimjia Yesu, nao wakasema, "Tumetumwa kutoka kwa Yohana. Je! tumtazamie mwingine, ama ni vipi?"

32 Akasema, "Kaeni tu na mwone kinachotukia." Ndipo, basi, wakangojea. Wakapanda mlima wakarudi.

33 Yesu akawaangalia. Akasema, "Mlitoka kwenda kuona nini, mlipoenda kumwona Yohana; mtu, mavazi mororo?" Kasema, "Wako kwenye majumba ya wafalme." "Mlienda kuona unyasi unaotikiswa na upepo wowote?" Si—si Yohana. Kisha Yeye akasema, "Vema, mlienda kuona nini; nabii?" Kasema, "Nasema, na zaidi ya nabii. Kama mnaweza kulipokea, huyu ndiye aliyenenwa habari zake, 'Namtuma mjumbe wangu mbele ya uso Wangu.'" Malaki 3.

34 Kisha wakinena kumhusu Yohana wakati mmoja, wale wanafunzi walisema, wakati alipokuwa akizungumza kuhusu mahali ambapo Yeye alikuwa akipanda kwenda Yerusalemu kutolewa, wao walisema, "Vema, ni kwa nini tunafundishwa katika Maandiko, na waandishi, ya kwamba Eliya hana budi kuja kwanza na kurejesha mambo yote?"

Akasema, "Eliya ameshakuja tayari, nanyi hamkujua."

35 Sasa angalieni. Kwa hao waandishi. . .Mwaweza kunisikia? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hao waandishi, hata hao mitume, ambao, ishara yao ya mwisho kabisa, ilikuwa ni kumtazamia Eliya. Hebu nirudie hilo. Walikuwa na Wateule wenyewe, waandishi na mitume, walioitwa na Bwana, waliokuwa wakimtarajia Masihi kuja, bali Eliya aje na kukutangulia kuja Kwake. Ndipo akaja, na—na kukufanya kwa unyenyekevu sana, na. . .mpaka hata wao hawakumtambua.

36 Basi hebu niseme hili, kama wazo langu mwenyewe, moja ya siku hizi. . .Mnatazamia mengi kutukia, ambayo yanatukia nanyi hamjui. Mnaenda kusema, "Kabla ya Unyakuo wa Kanisa. . ."

37 Sasa sipo hapa nikihubiri fundisho. Wapo wahudumu jukwaani hapa, ambao labda wasingekubaliana na Hili. Karibu wahudumu wote wanaamini ya kwamba Kanisa litapitia kwenye wakati wa Dhiki, kwa ajili ya utakaso; siwezi kuliona. Damu

ya Yesu Kristo ndiyo utakaso wetu; hakuna kilicho safi zaidi, mnaona. Mnaona? Ninaamini ya kwamba kanisa, kanisa la kimadhehebu na mwanamwali aliyelala, kweli wanapitia kwenye ile Dhiki, bali sio Bibi-arusi. Ipo tofauti kati ya kanisa na Bibi-arusi. Bibi-arusi anaenda katika Unyakuo. Hapo ndipo ninyi church of God, la Anderson, mlipochanganyikiwa kabisa kule juu, mnaona, ni katika hilo.

38 Sio kusema, kuwaambia kile mlichofanya ama hamkufanya; sipaswi kusema hayo, bali ni mahali tu jinsi ninavyoliona. Kitu cha kwanza mnajua, mnaenda kusema, "Mbona, nilidhani kulipaswa kuwe na Unyakuo kabla ya Dhiki."

39 Ile Dhiki itapiga. Basi itakuwa ni kitu gani, kibaya sana, kama ukisikia ikisemwa, "Umeshatokea tayari wala hamkujua"?

40 "Mmoja atakuwa shambani, nitamchukua mmoja nimwache mmoja," mtu fulani kukosekana tu. Kutakuwako na wachache, wachache sana katika Unyakuo huo, watakaobadilishwa. Bibi-arusi aliyelala, Bibi-arusi ambaye amechukuliwa kote katika wakati, Yeye atatokea kwanza. Ndipo basi sisi tulio hai na tuliosalia tutanyakuliwa pamoja nao, mmoja tu *hapa*, na mmoja *pale*, na mmoja *huku*.

41 Angalau, kila siku kote ulimwenguni, kunao watu wengi wapatao mia tano wanaokosekana. Na vipi kama kuna elfu moja? Wao wangesema, "Loo, vema, mwanamke huyu, alitoroka tu na mtu fulani. Mhubiri huyu, alimchukua mke wa mtu mwingine, na kuondoka." Ameenda Utukufuni, katika Unyakuo, na wao hawatajua.

Hivi Yeye hakusema Yeye "angekuja kama mwizi usiku"? Mnaona?

42 Unasema, "Vema, kama akija Yeye, nitamwona." La, la. Wale tu watakaomwona Yeye wanaenda kumwona Yeye kwenye wakati huo. Mnaona?

43 Mnaona, ni kama tu ile Nuru, kama vile Yohana alivyosimama pale na kuiona hiyo, yule Roho wa Mungu, kama Nuru, hua, akishuka na kuenda juu Yake, Sauti ikisema, "Huyu ni Mwana Wangu mpendwa," hakuna mtu aliyesikia Hiyo au kuiona Hiyo, ila Yohana. Mnaona?

44 Basi wakati huo Unyakuo utakapotukia, utakuwa ni badiliko. Na jambo la kwanza unajua, badiliko hilo, halafu tutanyakuliwa ndani yao, na kuondoka. Na yule mwanamwali aliyelala, anaendelea tu moja kwa moja vivyo hivyo, na kufikiri kila kitu kinaendelea vizuri. Nao tayari wameondoka, "Umetukia tayari, wala hamkujua."

45 Sisemi itakuwa hivyo, kumbukeni. Sisemi Bwana ananiambia itakuwa hivyo. Lakini ninaamini umekaribia sana, inawezekana. Sitaki kubahatisha hata kidogo. Ninataka kuwa tayari. Ninataka kila kitu tayari. Si—si—sitaki kamwe. . .

"Mzigo umewekwa kando," kama, jinsi unavyokuja. Labda vile tumeupangilia wote itakuwa vinginevyo, daima huwa hivyo, kuliko vile Yeye ni . . . tumeupangia. Kuja Kwake kwa kwanza kulikuwa hivyo, na Kuja Kwake kwa pili huenda kutakuwa ni jambo lile lile.

Hebu tuombe sasa. Na tuwe waaminifu.

46 Chicago, mnajua mimi ni Mkusini, nimezoea ukarimu Kusini. Mnalo jiji kubwa hapa, kubwa, jiji kubwa mno lenye watu milioni tano ndani yake. Bali sijui jiji lolote kubwa ulimwenguni ambalo kweli, kutoka kwa watu huku, ni watu wa kirafiki na wema kama watu katika Chicago. Hiyo ni kweli. Hawa watu wa Chicago ni watu wazuri. Hata unatoka nje hapa mtaani, na tulikuwa tukizungumza hata na walevi na kila kitu kingine, wao—wao wanakuheshimu, na ni wazuri. Kweli na—na—nathamini hilo.

47 Na hebu niwaambieni. Pamoja na ono hivi majuzi asubuhi, ninajua kwamba baadhi ya Bibi-arusi wanangojea hapa Chicago, kwa ajili ya Kuja kwa Bwana. Ninajua kutakuwako na kundi kutoka kwenye jiji hili, watakaonyakuliwa, kulingana na ono, ambalo halijawahi kushindwa. Na ninajua wako, Mungu anao watu hapa ndani ambao wanaenda katika Unyakuo huo, ni—ninaamini hilo, katika siku hiyo.

48 Nafikiri nimesema ya kutosha na nikaenda umbali wa kutosha, mpaka inanibidi kuacha kusema sasa, kwa hiyo hebu tuombe.

49 Bwana Yesu, tusaidie sasa tunapoliendea Neno. Jalia watu waelewe dhahiri, Bwana, ya kwamba wanadamu tuko pamoja. Tunajua kwamba tunachoka na kudhoofika. Na, bali naomba ya kwamba utatujalia mara moja zaidi, usiku wa leo, kulitikisa maskini kanisa hili, Bwana, kwa nguvu Zako, kwa Neno, na jalia kusiweko na mtu mnyonge miongoni mwetu.

50 Bwana, tunakushukuru Wewe kwa sababu kwamba tunaamini, kwamba tunapoomba mambo haya, tunayapokea. Ninaomba ya kwamba—kwamba—kwamba Wewe utafanya tu jambo kubwa miongoni mwetu, usiku wa leo, Baba. Katika Jina la Yesu ninajikabidhi mwenyewe, pamoja na fungu hili ninaloenda kulisoma. Pia ninaomba ya kwamba Wewe utalifunua Hilo kwetu kwa njia kuu, ili watu waweze kufahamu dhahiri. Amina.

51 Ninawatakeni, mkitaka, mngetaka wakati huu, na ni karibu . . . Nitajaribu kuumaliza hasa kwenye wakati, usiku wa leo, nikiweza, kuondoka mapema kidogo kuliko nilivyofanya jana usiku, kwa vyovyote vile. Lakini fungueni pamoja nami kwenye mla- . . . Injili ya Luka Mtakatifu. Ama, samahani, hebu tubadilishe hilo; nimeandika Luka hapa chini, lakini ni—nimefungua hapa pia kwenye Mathayo.

52 Mathayo, mlango wa 15, kuanzia kifungu cha 21. Marko Mtakatifu inatoa taarifa yake, pia.

> *Yesu akaondoka huko, akaenda kando pande za Tiro na Sidoni.*
>
> *Na tazama, mwanamke Mkananayo wa mipaka ile akatokea, akampazia sauti akisema . . . Unirehemu, Bwana, Mwana wa Daudi; binti yangu amepagawa na pepo.*
>
> *Wala yeye hakumjibu neno. Nao wanafunzi wake wakamwendea, wakamwomba, wakisema, Mwache aende zake; kwa maana anapiga kelele nyuma yetu.*
>
> *Akajibu, akasema, Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.*
>
> *Naye akaja akamsujudia, akisema Bwana, unisaidie.*
>
> *Akajibu, akasema, Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa.*
>
> *Yule mwanamke akasema, Kweli, Bwana, lakini hata mbwa hula makombo yaangukayo kutoka kwenye meza za bwana zao.*
>
> *Ndipo Yesu akajibu, akamwambia, Mama, imani yako ni kubwa; na iwe kwako kama utakavyo. Akapona binti yake tangu saa ile.*

53 Tunao hapa, tunaotafakari, usomaji mrefu sana wa Maandiko, nami sitaki kutumia wakati mwingi sana kwa huo. Ambapo, ungeweza kukaa usiku kucha, tuseme, mtu yeyote anajua, maana Maandio yote yametolewa kwa uvuvio. Ninaamini hilo. Bali nataka kuchukua neno moja, kutoa so—somo kutoka kwake. Nitaliita neno hilo: *Mng'ang'anizi.*

54 Neno *kung'ang'ania* linamaanisha "kushikilia," na kushikilia katika kutimiza lengo ama—ama kufanya jambo fulani. Na kila mtu, hiyo ni katika nyakati zote, aliyewahi—aliyewahi kufanya jambo lolote kutoka kwenye nafsi zao, au aliyefanya lolote, angekuwa mwenye kushikilia katika ja—jambo walilokuwa wanajaribu kufanikisha.

55 Na kabla hujaweza kuwa mng'ang'anizi, inakubidi kuwa na imani katika yale unayojaribu kufanikisha. Na ikiwa huna imani katika yale unayojaribu kufanya, kamwe hutaweza kuyafanya.

56 Sasa, hilo neno dogo, imani, linamaanisha mengi sana, na hata hivyo tunalishika kwa wepesi sana. Ninawasikia watu wengi sana wakisema, na kuingia, ni la kushangaza, wakisema, "Loo, nina imani!" Na pasipo kupuuza jitihada zao, bali unajua wakati mwingine wale wanaodai wana imani nyingi sana, ninakuta, wanayo kwa uchache kuliko wale wasiosema chochote juu yake. Wao, wamejijenga kwenye mhemuko, na si imani halisi.

Kuna tofauti kubwa, bali tumaini, mhemuko ulio na tumaini, kuliko kunyamaza na kutumia imani. Mnaona?

57 Imani ni kitu. Ni bayana. Si kitu ambacho—ambacho unakirukia tu, na kukigonga kiholela na kutumaini ndivyo. Ni kitu ambacho unakijua. Unacho. Ja—ja—jambo ambalo una—unaombea, hakuna njia ya kibinadamu ya kuelezea jinsi utakavyolipata, lakini hata hivyo unajua lipo. Unalo. Ni bayana.

58 Kama ningeweza kulipata hilo kusudi muweze kulielewa dhahiri, ingemaanisha mengi sana kwa mkutano huu usiku wa leo. Kama, katika usiku huu wa ibada hii ya uponyaji . . .

59 Ama, tunatumaini. Ni—ninasema hilo, "uponyaji," kwa sababu ninaamini ya kwamba Mungu ataponya. Ninaamini kwamba Mungu anaenda ku—kufanya yale Yeye aliyoahidi kufanya. Na kama sikuamini, ningehofia kusimama hapa katika kusanyiko hili la watu na kutoa matamshi haya ninayotoa. Kwa sababu, kama nilikuwa na woga mdogo kabisa kulihusu, afadhali kamwe nisiingie mlango ule.

60 Inakupasa kuliamini kabisa. Nawe una hakikisho, na hakuna kitu kinachoweza kulitikisa. Wewe, haijalishi kunafanyika nini, ungali unaliamini. Hata ingawa inaonekana kana kwamba limeshindwa, ungali unaliamini. Haijalishi kinachofanyika, ungali unaliamini.

61 Kama vile maskini mama huyu anayeketi hapa akiniangalia, hapa hivi majuzi usiku, Bibi Way alikuwa akimshughulikia.

62 Mume wake alifufuliwa hivi majuzi, kutoka kwa wafu, akifa kwa mshtuko wa moyo. Na mimi nilitoka jukwaani, na kwa sababu, nilipomwona, macho yake yalirudi nyuma na akafa, si—si—sikujua la kufanya, ndipo nikaenda pale chini kuuchunguza moyo wake na kumgusa. Basi, unaona, alikuwa ameaga, ndipo ikabidi niwe naye.

63 Halafu basi hivi majuzi usiku, niliulizwa swali, "Kwa nini hukushuka uende kwa huyo mama?" Aligeuka, ama Bibi Way alijaribu kumtoa nje. Naye akaanguka sakafuni, na uso wake ukageuka mweupe, na karibu tu ameaga. "Basi kwa nini hukushuka kwenda kule?" Kwa sababu kwamba sikuwa na sababu ya kwenda kule. Mnaona?

64 Imani si jambo ambalo mtu mwingine anajaribu kukufanya utende. Ni jambo ambalo Mungu anakuagiza kufanya. Mnaona? Mnaona?

65 Niliona mama huyo alikuwa tu . . . Alikuwa mgonjwa sana, bali ameleweshwa na dawa, sio . . . akijaribu kupata nafuu, daktari alikuwa amempa. Nami nilimwona ameketi, akicheka na kushangilia, basi kuna haja gani ya mimi kushuka kwenda kule wakati imekwisha tayari? Mnaona? Mnaona? Ndipo mtu fulani akasema, "Lakini Bw. Way angeninii, angeninii, angelala pale." Lakini ilibidi twende tukafanye hili. Lakini wakati mwanamke

huyo alikuwa amerudi nje, hata hivyo ono lilikuja. Naye ameketi hapa usiku wa leo, mzima; akicheka jana usiku. Naam.

66 Unaona, wewe, huna budi kujua. Na huwezi kujua mpaka uwe na imani, nayo imani husababisha huko kujua ndivyo ilivyo. Imani ni kule “kujua.” Imani ni kile kitu kinacholisema.

67 Sasa, sasa tunapokuona huku kung’ang’ania. Mtu yeyote anayejaribu kufanikisha kitu chochote, amekuwa mng’ang’anizi.

68 Kwa mfano, George Washington anaitwa baba wa taifa hili. Usiku mmoja aliomba usiku kucha, kwenye theluji. Na wakati Wamarekani wa kweli, halisi, wenye damu asili waliokuwa wameuchukua msimamo wao juu ya ardhi hii, na ule uchumi mkuu waliokuwa nao shirika ulikuwa hatarini, na kulikuwako na yapata asilimia sabini, ama zaidi, ya hao wanajeshi wa Marekani wamesimama huko nje, hata hawakuwa na viatu miguuni mwao. Miguu yao ilikuwa imeganda na kufungwa matambara, bali hata hivyo walikuwa na kiongozi waliyemwamini. Naye kiongozi huyo alimwamini yule Kiongozi, Mungu. Na aliomba mpaka nguo zake zikalowa, hadi kiunoni mwake, amepiga magoti kwenye theluji. Na hapo palikuwa na Delaware iliyoganda kati yake na mahali ambapo Waingereza walikuwa wakifanya mandhari yao—yao kwenye ng’ambo ya pili.

69 Bali Delaware yenye barafu haikumzuia njiani mwake, wala pingamizi yake ya wanajeshi wake walioganda, na miguu yao imeganda, na—na barafu mtoni. Aling’ang’ania. Alikuwa na imani kwamba Mungu alikuwa anaenda kumpa ushindi, na yeye . . . Dalaware isingemzuia njiani mwake. Naye akafanikisha kusudi. Ingawa risasi tatu za goboli zilipitia moja kwa moja kotini mwake; bali hazikumgusa. Alishikilia. Alikuwa amesikia kutoka kwa Mungu. Na alikuwa na imani kwamba yale Mungu aliyokuwa amemwambia yalikuwa ni kweli, wala hakuna kitu kingaliweza kumkomesha.

70 Kama kila mtu mgonjwa hapa ndani, usiku wa leo, angeweza tu kuwa na imani katika Mungu, kama George Washington alivyokuwa nayo; Dalaware yako, inayosimama mbele zako usiku wa leo, ingebidi iyeyuke na kutokomea, ungeivuka kwa njia fulani. Haidhuru ni nini upinzani wako, ungali ungeivuka. Ungeng’ang’ania, ung’ang’anie sana hata hiyo kansa, kivimbe, chochote kile, kisingeweza kusimama hapo, kwa sababu ungevuka uingie kwenye ahadi ambayo Mungu amekupa.

71 Wanadamu wanaweza tu kushikilia wakiisha ku—kusikia kutoka kwa Mungu. Imani imewekewa Msingi tu juu ya Neno la Mungu, maana imani chanzo chake ni kusikia Neno la Mungu.

72 Nuhu katika ule—ule upinzani aliohubiria, katika siku za wakati wake, katika kuandaa safina. Baada ya kumsikia Mungu

akimwambia ya kwamba Yeye alikuwa anaenda kuangamiza ulimwengu kwa maji, kwamba dhambi ilikuwa imelundikana juu sana hata asingeweza kuivumilia tena. Alikuwa anaenda kuufagilia mbali ulimwengu, kwa maji. Na hapakuwapo na maji hata kidogo angani, lakini hata hivyo Nuhu aling'ang'ania katika wakati wa wakosoaji. Haidhuru watu walimwambia kiasi gani, "Haliwezi kutukia," Nuhu alijua lilikuwa linaenda kutukia. Kwa sababu, na akiwa mng'ang'anizi!

73 Kamwe hakusema tu, "Vema, niliweka msingi wa safina, na—nadhani mimi. . .hilo, hilo litatosha, basi, kama sayansi tayari imethibitisha niko makosani."

74 Hivyo ndivyo watu wengi hufanya kuhusu kumjia Kristo. Wanaweka msingi, wa kumwamini Bwana Yesu na kumkubali Yeye kama Mwokozi wao binafsi, na labda kuendelea hata kwenye ubatizo wa Kikristo. Lakini inapofikia kule kufuatilia hadi mwisho, kufikia ubatizo wa Roho Mtakatifu, mtu fulani analieleza na kuliondoa kwao. Hiyo ndiyo sababu ile mbegu ilianguka kando ya njia, ama ilianguka penye mawe.

75 Lakini mwanamume na mwanamke walio na imani ya kwamba Mungu, ya kwamba Kristo, ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kwamba Neno Lake ni halisi tu sasa, na kila ahadi ni ya kweli tu kama ilivyowahi kuwa, hakuna mhudumu, hakuna mtu, hakuna mtu anayeweza kulielezea vinginevyo kutoka kwao. Wanang'ang'ania. Wanapanda mpaka wanafanikisha kile wamekusudia kufanya. Hakuna njia ya kulielezea na kuliondoa kwao. Wanaliamini.

76 Musa, yeye alifanya jambo lile lile, a—alikuwa amesahau lile ono na hisi za wale watu. Lakini wakati alipokutana na Mungu katika kile kichaka kilichowaka moto, naye akaona kwamba hilo lilikuwa ni Neno la Mungu! Mnaona, Musa ndiyo kwanza alelewe chini ya mafundisho mazuri, mama yake, na alikuwa amefundishwa njia ya Mungu. Bali wakati alipopanda kule na kukutana na Mtu huyu ambaye mama yake alikuwa amemfundisha kumhusu! Mnaona ninalomaanisha? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

77 Watu wengi huchukua Biblia na kuifahamu Hiyo, kikamilifu kiakili, lakini, hilo—hilo silo. Hilo silo tunalozungumzia. Haidhuru unaweza kuielezea Hiyo vizuri jinsi gani, huna budi kukutana na Mwandishi Wake, kibinafsi. Basi ndilo linaloleta imani, kwa kuwa huyo Mwandishi anaishi ndani yako ukiisha kuzaliwa na Yeye.

78 Musa alikutana na huyo Mwandishi, "MIMI NDIMI, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka na wa—wa Yakobo. Nami ninazikumbuka ahadi Zangu, na nimekuja kukutuma." Amina. "Ninakutuma wewe kuwakomboa."

79 Basi angalia wakati yeye alipofanya ishara yake ya kwanza, nayo ilionekana kana kwamba ilishindwa, kwa sababu alikuwa

na waigaji wengi. Wamisri wangeweza kufanya jambo lile lile alilofanya. Lakini, mnaona, Musa, baada ya kukutana na Mungu katika kichaka kilichowaka moto na kujua Huyo alikuwa ni Mungu, haikuleta tofauti yoyote ni wengine wangapi walioiiga na walikuwa ni watu wa aina gani walioiiga, Musa alijua ya kwamba yake ilikuwa ni ya kweli, ya kwamba ilitoka kwa Mungu. Alisimama tu kimya, mbele ya Farao, ndipo nyoka wake akala hao wengine.

80 Hivyo ndivyo watu wafanyavyo leo hii. Huenda wakawa . . . Kama hawana hakika, kama wamechochewa katika mhemuko fulani, nao wamwone mtu mwingine akienda mbali sana katika kilindi cha kitu fulani, na kuendelea, ndipo wanawazia, "Vema, labda yangu . . . "

81 Lakini—lakini mtu yule ambaye amekutana na Mungu kweli, na anajua hilo, anajua kile kilichotukia. Hilo, ni Mungu! Hakika. Hakuna mtu angaliweza kulielezea vinginevyo kutoka kwake.

82 Daudi, maskini, jamaa mwekundu, hakuwa mkubwa vya kutosha kubeba silaha, au upanga, hasa, katika siku hiyo, ngao yake. Alikuwa, alikuwa ni mdogo mno. Ilitokea kwamba yeye, kile ambacho tungekiita, duni. Naye baba yake asingeweza kuwa na chochote kwake kufanya. Yeye . . . ndugu Zake walikuwa ni watu wakubwa, warefu wenye nguvu. Kwa hiyo alifikiri angeweza kumtafutia Daudi kazi, labda ya kuchunga kondoo. Basi jamaa huyo mdogo akakaa huko nje, ndipo—ndipo akakutana na Mungu. Na yeye—yeye alikuwa na . . . Aliagizwa kuwachunga hao kondoo.

83 Naye Daudi alikuwa ni nabii, nalo Neno la Bwana lilimjia katika nyimbo. Naye Yesu alisema, "Hivi hamjasikia, katika Zaburi?" Jinsi mambo yalivyotabiriwa juu Yake, mwajua. Basi Daudi alikuwa mwandishi wa ki—kinabii wa nyimbo. Basi wakati alipokuwa huko nje, akiangalia juu, na kusikia upepo ukipita kwenye milima na chini kupitia mizeituni, aliandika kuhusu "malisho ya majani mabichi, yenye kivuli, na maji matulivu," na kadhalika, kwa uvuvio. Wakati alipoiandika usiku, akiziangalia nyota na mwezi, na—na jinsi maumbile yalivyotenda kazi, Mungu akamtembelea. Naye alijua kulikuwako na Mungu.

84 Basi siku moja, dubu akaingia na kumchukua mmoja wa kondoo zake. Na alimthamini sana kondoo huyo kwa sababu alikuwa amejifunza kumpenda kondoo huyo. Na yeye—yeye alimpenda. Na kwa hiyo wakati dubu alipoingia na kumshika mmoja, moyo wa Daudi ulianza kuwaka, wakati alipomsikia maskini kondoo huyo akilia. Naye Mungu alikuwa amemtuma kuwachunga hao kondoo. Na kwa hiyo wakati dubu alipomshika maskini mwana-kondoo huyo, naye akaanza kulia; Daudi, mara ghafla, alikumbuka ya kwamba Mungu aliyeumba mlima alikuwa ni Mungu wake. Kwa hiyo akatia jiwe kwenye

kombeo lake dogo na akamwandama dubu huyu mkubwa mkali, nalo likamgonga huyo dubu, naye akaanguka chini. Halafu, aliporudi, alikuwa na furaha kwa sababu alikuwa amepata ushindi.

85 Ndipo basi jaribu kubwa zaidi likaingia, simba, ambaye ni mkali sana kuliko vile dubu angekuwa. Anatisha zaidi. Na kama ningalikuwa na wakati, ningetaka kuwachambua hao wanyama na kuwaonyesha ule mfano mkubwa mle ndani. Basi simba akaingia na kumnyakua mmoja na kutoroka. Kwa hiyo kama Mungu aliweza kumpa ushindi dhidi ya dubu, hakika Yeye angeweza kumpa ushindi dhidi ya simba.

86 Loo, kama Mungu, Yule anayeweza kunipa ushindi juu ya nafsi yangu, amina, hakika anaweza kunipa ushindi dhidi ya ugonjwa unaojaribu kuniondoa Kwake. Mungu anayeweza kuniokoa na kunifanya kitu nisicho mimi; wakati nikiwa si Mkristo, anaweza kunifanya Mkristo, kwa kuliamini Neno Lake.

87 Basi, tunaona kwamba alimpata huyo dubu. Na hatimaye lile shindano kubwa la kuamua likaja, wakati a—alipotokea dubu mkubwa mkali mno, mkubwa kuliko hao wengine, alikuwa jitu la mtu. Basi Daudi alijua ya kwamba, akiwa na Mungu, alimshinda kabisa, haijalishi upinzani ulikuwa mkubwa jinsi gani. Akiwa na Mungu, yeye ni zaidi ya mshindi. Hata hivyo, mtu aliye mdogo kuliko wote, na mtu aliyepungukiwa na silaha sana; si mtu wa vita, mtoto; wala hana silaha, mwili wake m—mtupu tu; hana ngao juu yake, bali amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo. Na hakuwa na mkuki wala upanga, alikuwa na kombeo dogo; mwajua, vipande viwili vidogo vya kamba vyenye ngozi nchani. Basi alitaka kupigana na mtu huyo kwa sababu alikuwa akijaribu kuwaandama kondoo wa Mungu. Na kama Mungu angeweza kumwokoa kondoo, ni zaidi sana vipi familia Yake, watu Wake!

88 Chicago, hiyo ndiyo sababu sisi tupo hapa, nyinyi ni zaidi ya kondoo. Ninyi ni watu wa Mungu. Wala hatuna msomi wala dhehebu kubwa mno nyuma yetu. Lakini tunajua ya kwamba maradhi yamewashika, nanyi mmenaswa katika—katika masumbuko ya ulimwengu, nasi tunakuja katika Jina la Bwana Yesu. Ingawa daktari atakukatalia mbali, hatujali kile amefanya; tumekuja kukurudisha kwenye afya, katika Jina la Yesu Kristo, kwa kombeo dogo, la Neno Lake. Kamba mbili ndogondogo, Agano Jipya na la Kale, yakimshikilia Yesu kati yake, nasi tunakuja kukurudisha mahali pako, kama tu utaturuhusu.

89 Mtazameni maskini Samsoni, pia, kama nilivyonena kumhusu jana usiku, mwenyewe alikuwa mng'ang'anizi sana, mradi tu angeweza kuhisi vile vishungi saba vikining'inia mgongoni mwake. Wa—Wafilisti hawakumaanisha chochote kwake, haijalishi kama hakuwa na kitu ila mfupa wa taya la

nyumbu mkononi mwake, ama chochote alichokuwa nacho. Wafilisti, ama malango ya Gaza, hayakumaanisha chochote kwake. Mradi tu angeweza kuhisi hivyo vishungi saba, hilo lilikuwa ndilo agano.

90 Na mradi tu Mkristo anaweza kuhisi hilo agano, "mambo yote yanawezekana kwake yeye aaminiye," unapoweza kuhisi hiyo imani ya agano ndani yako, kwamba wewe ni mwana wa Mungu na mrithi wa kila moja ya baraka Zake zilizoahidiwa. Sijali kinachoinuka, wewe ni zaidi ya mshindi kwake, mradi tu unaweza kuhisi na kujua ya kwamba unaliamini. Mnanifuata? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mradi tu unaweza... Samsoni alipovihisi hivyo, a—alikuwa sawa. Na mradi tu, moyoni mwako, kwamba hujachochewa tu, huna mhemuko, bali moyoni mwako unajua ya kwamba unaenda kulipata. Unajua ya kwamba umekiri dhambi zako, unajua ya kwamba umepita kutoka mautini kuingia Uzimani, unajua ya kwamba wewe ni mtoto wa Mungu, mrithi wa mambo haya, basi hakuna kitakachokuzuia kulipata. Basi wewe ni mng'ang'anizi.

91 Yohana Mbatizaji aling'ang'ania sana hata akatoa tamshi hili. Miaka elfu nne walikuwa wamemtazamia Masihi, bali Yohana alijua ya kwamba alikuwa anaenda kumtambulisha Huyo. Alijua ya kwamba alikuwa na... Yesu alisema alikuwa ni zaidi ya nabii. Alikuwa nabii, bali alikuwa ni zaidi ya nabii, kwa sababu alikuwa ndiye mjumbe wa agano. Naye alikuwa na hakika sana na hilo, kwamba alikuwa anaenda kuiona hiyo Nuru, huyo Hua. Alikuwa anaenda kumwona huyo Roho. Alikuwa na hakika sana nalo, hata akasema, "Kuna wengine waliosimama, Mmoja anayesimama kati yenu sasa, ambaye hamumjui. Sistahili kuvifungua viatu Vyake; bali Yeye atakuwa Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto." Mungu alikuwa...

92 Yeye alikuwa ni nabii, na zaidi ya nabii, na alijua agizo lake. Alijua ya kwamba Mungu alikuwa amemwagiza, na hapakuwapo na hofu moyoni mwake. Ingawa ni miaka elfu nne, katikati ya umati mjeuri wa wakosoaji, wakimdhihaki, na kusema yeye, alikuwa mtu wa msituni akijaribu kuwazamisha watu, hilo halikumkomesha hata kidogo.

93 Huenda mtu fulani alisema, "Yohana, hivi huogopi kwamba halitatukia?"

94 Lingewezaje kushindwa wakati Mungu alisema hivyo? Mungu alimwambia, "Yule utakayemwona Roho akishuka juu yake, na kubaki juu yake, Huyo Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu."

95 Yohana alijua hilo. Hakuogopa kushindwa. Huo ulikuwa ndio wajibu wake, hilo lilikuwa ndilo agizo lake, kwa hiyo angeweza kung'ang'ania sana, kushikilia sana. Haidhuru, hakuna kitakachomsumbua. Hapakuwepo na pepo wa kutosha

kutoka matesoni wangeweza kumchukua. Haleluya! Aliagizwa kufanya jambo fulani. Na mbingu na nchi zitapita, bali Neno hilo halitashindwa kamwe. Yeye alisema, "Nitamwona Huyo!" Sasa imani ilikuwa imetia nanga.

96 Alikuwa amesikia kama Musa, huko nyikani, ambako manabii wana—wanafinyangwa. Alikuwa amemsikia Mungu akimwambia, "Wewe ni sauti ya mtu aliaye nyikani. Ninaweza kukuelekeza kwenye Maandiko na kukuonyesha agizo lako. Wewe ndiwe Isaya alisema, miaka mia saba na kumi na miwili iliyopita, 'Kutakuwako na sauti ya mtu aliaye nyikani.'"

Wao wakasema, "Je! wewe ndiwe Masihi?"

97 Akasema, "La. Bali mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani, 'Yatengenezeni mapito ya Bwana, zinyosheni njia Zake!'" Naye alijua ya kwamba alikuwa anaenda kufanya hivyo, kwa sababu Mungu alisema hivyo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Imani, kisha aling'ang'ania.

98 Marabi, na kadhalika, wakatokea, kasema, "Unamaanisha wakati utakuja ambapo dhabihu ya kila siku itaondolewa? Mtu atachukua mahali pake, na kadhalika?"

99 Akasema, "Yuaja Mtu atakayepachukua mahali hapo, na Yeye ataondoa dhabihu za kila siku. Atakuwa ni Mwana-kondoo." Na wakati alipogeuka kuangalia, akasema, "Tazama, Yule pale, yule pale Mwana-kondoo wa Mungu aziondoaye dhambi za ulimwengu," moja kwa moja katikati ya mahubiri yake, kwa sababu Mungu aliahidi Huyo.

100 Haijalishi wanasema nini, "Vema, watakutupa gerezani. Shirika la wahudumu litakufukuza. Hutakuwa na ushirika wowote. Hamna ushirikiano."

101 Halikuleta tofauti hata kidogo kwa Yohana. Aling'ang'ania. Alikuwa na ujumbe, mtu fulani hana budi kuusikia. Na kutoka kwenye kundi lake lote, sidhani alipata yapata kumi na wawili, bali alipata kitu.

102 Wakati alipopata nguvu za Mungu juu yake, ndipo Bwana akaanza kutenda kazi juu yake. Sasa, Bwana Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Wakati tunapoweza kuliona agizo la Bwana, basi unaweza kung'ang'ania.

103 Jamani, maskini mwanamke huyu Myunani, alikuwa amesikia habari Zake. Kamwe hakuwa amemwona Yeye, bali alisikia tu kumhusu Yeye. Alikuwa amesikia sifa Zake.

104 Vema, tunasikia jambo lile lile. Tunasikia sifa Zake. Tunasoma juu ya sifa Zake. Tunaona sifa Zake. "Nayo imani chanzo chake ni kusikia." Kwa njia moja, ama nyingine, imani hupata chanzo ambacho wengine hawaoni. Wakati umekusudiwa tangu zamani kwa kitu fulani, unaweza kukiangalia moja kwa moja, kwa sababu imani yako

inakitangaza, na wengine hawajui chochote juu yake. Imani hupata chanzo hicho ambacho huwezi kuona.

105 Maana, wengine wanakitazama kwa kuchunguzachunguza, na kadhalika. Nao wanakiangalia, wakidhania. Nalo neno *dhania* ni "kudiriki pasipo mamlaka."

106 Naye Musa kamwe hakushuka kwenda Misri, akidhania ya kwamba Mungu alikuwa pamoja naye; alishuka kwenda Misri akijua Mungu alikuwa pamoja naye. Mnaona? Huukubali uponyaji wako, ukifikiri Mungu atakuponya. Unaukubali uponyaji wako maana Mungu tayari ameutimiza. Yeye aliahidi jambo hilo, na imani yako inasema ndivyo lilivyo, na hakuna kitu kingine kinachoweza kulifutilia mbali.

107 Sasa, Neno Lake ni upanga, Biblia ilisema. Katika Waebrania 4:12, Ilisema, "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, Hilo hutambua mawazo yaliyoko moyoni." Hilo ndilo Neno lifanyalo.

108 Sasa kitu pekee kinachoweza kuutumia upanga huu ni mkono. Na kitu pekee kinachoweza kulitumia Neno la Mungu ni imani. Kama Neno ni upanga, basi imani inaushika, inaukamata sana. Basi wakati watu wanapopambana, kama vile watu wawili wakikutana, na kwa visu hivi wana—wanapambana. Huyo ni wewe, na ibilisi akijaribu kukufanya utilie shaka. Sasa, upanga wako ulio nao, huenda ukawa mzuri sana, ni mzuri kuliko wake mara milioni moja. Nitakwambia, wake hata si upanga, ni fimbo. Bali wako ni upanga. Lakini kama mkono unaoushika upanga huo ni dhaifu, hiyo fimbo inaweza kuushinda. Lakini haidhuru mkono huu ni mdogo vipi, kama ukilishika Neno la Mungu, kwa imani, hakuna kitu kitakachoushinda. Unaweza kuangusha chochote.

109 Unaona, yeye anaushika kwa mkono wake wa kulia, nawe katika mkono wako wa kulia; basi panga zenu zinaposhikamana, unaposhikamana na ibilisi, "Hilo ndivyo lilivyo, ama sivyo?" Sasa anakusukuma, "Sema Hilo ni kosa, Hilo ni kosa! Haikupasi kuliamini Hilo."

110 Lakini laiti ungaliamini Hilo! Unaona, panga hizi zinakuja moja kwa moja hata kwenye mipini. Sasa kama ninaweza kuusukuma wake nyuma, kwa mpini wangu, ubapa, namna hiyo, niko wapi? Nimeuelekeza moja kwa moja moyoni mwake, maana niko upande mzuri, mkono wake wa kushoto. Na basi ninaposukuma kwa imani, kwa Neno, "Shetani, Yesu Kristo aliniagiza kufanya hivi," nasi tunashikamana. Na kuinuka kwa mkono huo wa imani, na kusema, "Malaika wa Mungu alikutana nami huko, na akasema Hilo ndivyo lilivyo." Muda si muda wajua, ninaingiza upanga moja kwa moja ndani, naye ameshindwa. "Nimekuja kukukabili! Na BWANA ASEMA HIVI." Huyo ni mwaminio, wakati akiwa na imani kulishika Neno.

111 Sasa kama wewe ni maskini mnyonge tu wa kimadhehebu, afadhali usiikaribie; utazungukazunguka, uzungumze habari zake, na kusema haliwezi kutukia, kwa sababu hujui chochote kulihusu. Lakini mtu huyo ambaye amelitumia, na kuliona likimshinda huyo adui, anajua litakachofanya.

112 Huyu maskini, mwanamke mdogo, kamwe hakuwa amemwona Yeye, bali alikuwa amesikia habari Zake. Alikuwa na vizuizi vingi, ila imani yake haikuwa na kizuizi chochote. Imani haina kizuizi chochote hata kidogo.

113 Huenda ukawa na vizuizi vingi. Huenda ukawa na neno la daktari, mwanasayansi ambaye amekufanyia uchunguzi. Huenda ikawa kwamba yeye, mtu huyo, alikwambia, "Wewe, utakufa." Hayo ndiyo yote ajuayo. A—amekwambia yote aliyojifunza. Kazi yake ya kisayansi inaonyesha ya kwamba, ya kwamba huna budi kufa. Mfumo wako wote umefanywa kwa njia ya namna hiyo, kwamba mauti yameupiga, na hakuna kitu kinachoweza kuyazuia kuendelea. Unaenda. Sasa, hayo ni kadiri ajuavyo. Hakuna sayansi iliyo na dawa yoyote kwa ajili yake.

114 Bali umepata kitu fulani. Unachukua ule upanga. Unaona? Sasa, hakika, una kizuizi, una kitu kitakachokushambulia: huyo ibilisi, huo ugonjwa, mateso hayo. Lakini utakapopiga ncha ya panga pamoja na ibilisi huyo huko, na kusema, "Ni BWANA ASEMA HIVI! Alinifunulia, nami nimeponywa!" Loo, jamani! Imani yako haina vizuizi vyovyote.

115 Mnajua, hebu tuchukue baadhi ya vizuizi vyake, tukaviangalie, dakika chache tu kabla hatujaitisha mstari wetu wa maombi. Huenda walimwambia, kwanza kabisa, "Wewe ni Myunani; Yeye ni Myahudi." Vema, kwa maneno mengine, huenda ilisemwa, "Unajua, dhehebu lako haliudhamini mkutano huu. Kanisa lako haliudhamini." Lakini, unajua, hilo halikumzuia. Imani ilikuwa tayari imegonga. Alikuwa amesikia kuhusu mtu mwingine kuponywa. Naye alikuwa na haja, na kitu fulani kikamwambia ingewezekana.

116 Sasa, unaona, kazi za Mungu zilikusudiwa kimbele na Mungu. Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

117 Yesu alikutana na kipofu wakati mmoja, kasema, "Ni nani aliyetenda dhambi, yeye ama mama yake, ama kadhalika, ama baba yake?"

118 Kasema, "Si hata mmoja wao, bali ili kwamba kazi za Mungu zidhihirishwe."

119 Mnaona, hili ni kazi za Mungu. Basi unaposikia kitu fulani kikikusukuma, kishikilie. Huyo ni Mungu akinena nawe.

120 Vema, yeye alikuwa angali anang'ang'ania ingawa walikuwa wamesema kwamba, "Wewe si wa watu Wake, na kanisa lako

halishiriki katika mkutano huu." Aling'ang'ania, kwa vyovyote vile. Alikuwa anaenda, kwa vyovyote vile.

121 Huenda aliteremka barabarani akakutana na kundi jingine la makuhani, na wao—wakamwambia, "Ngoja kidogo. Siku za miujiza zimepita. Huo ni u—udanganyifu mtupu. Hilo ni kundi tu la—la watu, mtu fulani anayejiita nabii kule chini akifanya mambo yote ya namna hii. Huo, unajua, huo, huo ni upuuzi tu. Mbona, hakuna kitu kama hicho leo hii." Lakini angali alikuwa mng'ang'anizi. Angali aliamini lilikuwa linaenda kutukia. Sasa, hapo ndipo unapoupata. Hapo ndipo jambo fulani linapotukia.

122 Huenda alishuka akaenda kwenye kona nyingine, akakutana na mume wake, naye mumewe akasema, "Kama ukienda huko chini na kujihusisha katika kundi hilo, nitakuacha." Vema, anaweza kuondoka akitaka, bali mwanamke huyo angali anang'ang'ania. Anang'ang'ania. Anayo haja, na imani tayari imetia nanga. Anajua litatukia.

123 Kuteremka chini kwenye kona nyingine, akakutana na kundi la watu, na kusema, "Unajua nini? Utakuwa ndiye kichekesho cha mjini, ukishuka kwenda kule kuomba rehema kwa ajili ya binti yako. Nawe utakuta kwamba si zaidi ya vile wengine wameomba na hawakupata." Haileti tofauti yoyote kile wengine walichofanya, na kama wengine walichekwa, angali aling'ang'ania. Alijua lililokuwa linaenda kutukia. A—aliamini. Alikuwa amesikia habari Zake. Alijua, kama angewahi kufika pale, kile kilichokuwa kinaenda kutukia.

124 Sasa huenda tulishuka tukaenda pembeni na kukutana na mchungaji, naye akasema, "Utafukuzwa kutoka kanisani mwako kama ukienda." Angalia kizuizi maskini mdogo huyo alichokuwa nacho. Pia kumbukeni, yeye ni Myunani, sasa, si Mpentekoste. Naye huyu hapa anashuka anaenda, nao wakasema, "Utafukuzwa kutoka kanisani mwako." Na angali alishikilia.

125 Aling'ang'ania. Haikuleta tofauti yoyote kama alimpoteza mume wake, aliwapoteza rafiki zake, alikuwa ndiye kichekesho cha mjini, na chochote kilichotukia, ama hata alifukuzwa kanisani mwake, ama chochote zaidi. Imani ilikuwa imeshikilia! Aling'ang'ania. Ninapenda hilo.

126 Sasa, watu wengi hufikiria ya kwamba hayo ndiyo yote wanayopaswa kuwa nayo, mradi tu wamemfikia Yesu, na kuja mahali Yeye—Yeye alipo mkutanoni, vema, hilo tu ndilo linalohitajika.

127 Ilikuwa kwamba makanisa, wakati nilipoanza kwenda hudumani mara ya kwanza, wangeketi na kungojea, karibu walie, mpaka Bwana ajitokeze jukwaani, na, ndipo, loo, jamani!

128 Hapa chini Illinois, mahali padogo paitwapo. . .Loo, ninasahau mahali palipo sasa; katika mmoja wa mikutano yangu hapa chini, miaka iliyopita, ambapo Chicago Tribune

hapa ilichapisha makala kwamba kulikuwako na magari ya kuchukulia wagonjwa ishirini na saba karibu na hoteli hiyo ndogo. Ndipo usiku mmoja, huku nikitembea kwenda jukwaani, nikiweka msingi wa yapata dakika thelathini, na kuwaomba watu, na kuwasahi waamini. Ndipo kwa ombi moja kutoka jukwaani, Bwana akiisha kujifunua Mwenyewe, kwamba Yeye alikuwako, hapakuwapo na . . . hapakuwapo na mtu kwenye kiti cha magurudumu au kitanda cha wagonjwa, kiziwi, bubu, au kipofu, popote. Kila mmoja wao aliponywa mara moja.

129 Durban, Afrika Kusini, tuliona wenyeji elfu ishirini na tano wavaao blanketi wakiponywa wakati mmoja, pamoja na malori saba yaliyojaa mikongonjo na magongo na mbao, ambazo walikuwa wamewabebea, yakiteremka mtaani, nao hao watu wakitembea nyuma, wakiimba *Amini Tu*.

130 Imani! Yaondokee ma—mawazo yako. Waza mawazo Yake. Unaona? Waza kile Yeye awazacho.

131 Unasema, "Ndugu Branham, ni—ni—nitaenda, nafikiri . . . " Huna wazo lolote linalokuja. Acha nia iliyokuwamo ndani ya Kristo iwe ndani yako, ndipo utalitambua Neno. Unaona? Tazama.

132 Wakati watu hao wangeketi na kungojea, wakati Bwana alipokuja na kufanya jambo fulani, loo, jamani, walisimama tu na kuondoka.

133 Lakini, unajua, inaonekana kana kwamba leo hii, wameona mengi sana yake. Na sasa Bwana anakuja . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Vema, anajionyesha Mwenyewe miongoni mwetu, tunasema, "Jina la Bwana libarikiwe. Hakika anaweza kutenda hilo. Ndugu Branham, ninaenda huko kwa Oral Roberts juma lijalo na kumwomba aniombee, na *hivi-na-vile*. Hili lisipofanikiwa, usiku wa leo, itanibidi . . . " Karibu huo ndio mtazamo tu, mnaona. Watu hawang'ang'anii.

134 Kama Roho Mtakatifu, kama Yesu Kristo, akithibitisha kwamba Yeye yuko hapa miongoni mwetu, basi kazana mpaka umfikie Yeye. Kama maskini yule mwanamke aliyekuwa anatokwa na damu, na mambo yote mbalimbali yaliyotukia, na maadui wote njiani mwake, alikazana moja kwa moja mpaka akamgusa Yeye. Ikiwa kanisa hili, usiku wa leo, lingefanya jambo lile lile, lingekazana kupenya kupitia kila kiwango cha kutokuamini, lingeshikamanisha panga na ibilisi na kutokuamini kwake, na lijitahidi kujua kwamba wewe ni mwana wa Mungu na mrithi wa mambo haya, na Yesu Kristo akiwepo kuwaonyesheni ya kwamba Yeye yuko pamoja nanyi, kulitimiza Neno Lake. Ng'ang'ania, usiache chochote kikuzuie.

135 Ninashangaa tu. Kama imani kweli ikitia nanga, kitu chochote kingeweza kukuzuia? Hamlipati. Kama kweli mlilipata, hilo lingetosha. Hivyo tu. Unaona?

136 Mwanamke huyu hapa, maskini, rafiki yetu Myunani, usiku wa leo, tuliye naye hapa mbele zetu, kama somo, wakati alipomfikia Yesu. Kama vile Yesu angewasili hapa pamoja nasi usiku wa leo; tuwasili, na Yeye aje hapa na kuthibitisha, Yeye huyu hapa miongoni mwetu. Vema, alidhani hilo lilitosha. Hilo halitoshi. La, bwana. Hapo ndipo wakati ndio tu umeanza kupiga vita. Huo ndio wakati tu unapoanza vita vyako halisi. Wakati alipofika kwa Yesu, ndipo Yesu aliposema hakutumwa kwa jamii yake. Loo, jamani!

137 Na jambo jingine, Yeye aligeuka na kuiita jamii ya watu wake si kitu ila kundi la mbwa. "Sijatumwa, ila tu kwa kondoo waliopotea wa watoto wa Israeli." Hilo halikumkomesha. Angali aling'ang'ania. Kisha kasema, "Isitoshe, si haki Kwangu kuchukua chakula cha watoto na kuwatupia ninyi mbwa." Angali aling'ang'ania.

138 Loo, napenda hilo. Angali alishikilia. Amina. Napenda hilo. Lishikilie! Yeye aling'ang'ania. Hakuwa mmea wa tuta la kuoteshea, ilibidi abembelezwe. La, bwana. Hakuwa chotara, kama sehemu kubwa ya mimea leo hii. Haikukubidi kumsihi na kusema, "Sasa, dada, nitakwambia, ningekutia moyo uendelee, kwa sababu. . . " La, bwana, hapakuwapo na mtu pale wa kumtia moyo, bali hata Yesu Mwenyewe alijaribu kumvunja moyo. Whiu! Utukufu! Sasa ninajisikia kama mtakatifu anayejibingirisha, hakika kabisa. Hata Kristo Mwenyewe akisimama pale, akijaribu kumvunja moyo, bali yeye alishikilia. Amina. Mng'ang'anizi! Alikuwa amefikia kitu fulani. Alijua hivyo.

139 Vipi kama Yeye angekuita mbwa, na jamii yako, kundi la mbwa? "Enyi kundi la Wachikago, enyi—enyi kundi la Wamethodisti, ninyi Wapresbiteri, hata sikutumwa kwenu. Ninyi si kitu ila kundi la wanafiki, hata hivyo." Whiu! Jamani! Ungeinua pua yako juu na kugeuka utokee kwenye mlango ule. Unaona? Kwa nini? Kamwe hujawahi kuwa na imani, kwanza kabisa. Wewe ni chotara, mmea wa tuta la kuoteshea ambao inabidi kunyunyiziwa wakati wote.

140 Sio mwanamke huyo! La. Jambo fulani lilitukia, imani ilikuwa imetia nanga. Hatashindwa. Amina. Haya basi. Haijalishi wengine wote wamefanya nini, kile wengine walichosema; yeye hatashindwa. La, bwana. Hata Yesu, Mwenyewe, asingeweza kumvunja moyo. Amina.

141 "Lakini sijatumwa kwa jamii yako. Nenda zako, potelea mbali, shuka uende barabarani. Sijatumwa kwenu nyinyi watu. Na nyinyi si kitu ila kundi la mbwa, hata hivyo. Mimi si . . . Kweli si haki Kwangu kukichukua chakula cha watoto na kuwapeni enyi kundi la mbwa, mbwa wa vichochoroni, panya wa mtaani, na kadhalika. Si—si haki Kwangu kufanya hivyo."

Ati nini? Alikubali ya kwamba Yeye alikuwa sahihi. Amina. Loo, jamani!

142 Imani daima itakubali Neno ni kweli. Kama mchungaji wako anasema hivyo au la, kama mtu yeyote anasema hivyo au hasemi, imani yako inasema Hilo ni kweli. Utukufu! Imani yako inasema Hilo ni kweli.

143 Kwa hiyo kile alichoitwa, hata na Yesu Kristo, Yule aliyemjia, na Yeye akamkemea. Pia waangalie wanafunzi Wake, watu waliokuwa pamoja na Yeye katika miamsho Yake, walisema, “Loo, potelea mbali! Ondoka hapa. Utatukasirisha. Usimsumbue Bwana wetu.”

144 Hilo halikumkomesha. La, bwana. Hakuna kitu kitakachomkomesha, maana anayo imani. Litatukia, kwa vyovyote vile. Alikubali Yeye alikuwa sahihi. “Mimi si kitu ila mbwa. Si—sistahili chochote. Lakini, Bwana, hebu nikukumbushe jambo fulani. Mimi siutafuti mkate; ninataka tu makombo machache.”

145 Shida yake sasa, hatuna watu wanaojinyenyekeza wapate makombo machache. “Sikuingia mstarini.” Hilo halileti tofauti yoyote. Nimekuja tu kuona kama Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ninatafuta makombo machache.

146 Loo, jinsi alivyokuwa tofauti na wakati huu. Kumbukeni, hakuwa amewahi kuona mwujiza. Alikuwa ni Myunani. Hakuwa ameona mwujiza kamwe, hata hivyo aling’ang’ania kwa sababu kitu fulani ndani yake kilimwambia alikuwa anaenda kuona mmoja.

147 Alikuwa ni kama Rahabu, yule kahaba. Rahabu, yule kahaba, yeye hakusema, “Sasa hebu mleteni Yoshua hapa, enyi wapelelezi, na hebu nione jinsi anavyovalia nguo zake, na aina ya tabia alizo nazo. Na hebu nione kama ana sura nzuri ama sivyo, ama jinsi anavyozichana nywele zake, kama ni mtu nadhifu na kila kitu.” Kumbukeni, kidogo hiyo ilikuwa ndiyo aina ya kazi yake, mwajua, alikuwa akiwawinda wanaume wenye sura nzuri, alikuwa kahaba wa mtaani. Basi kwa hiyo akasema, “Nimesikia ya kwamba Bwana Mungu yuko pamoja nanyi, nami ninaomba rehema.” Loo, jamani! Haya basi, imani chanzo chake ni kusikia. “Nilisikia ya kwamba mlimchukua Agagi, na yale mliyofanya kule chini. Pia nilisikia yale Mungu aliyowafanyia kwenye Bahari ya Shamu, nami ninaamini hayo. Pia ninajua kwamba ninyi ni watumishi Wake. Ninaomba tu rehema.” Amina. Alijaliwa rehema.

148 Mwanamke huyu, alipewa rehema. Alisema, “Kweli, Bwana, lakini mbwa hula makombo yaliyo chini ya meza ya bwana.” “Kwa msemo huu . . . ” Hilo lilitosha. Hatimaye, kwa kushikilia, kung’ang’ania, kutoruhusu chochote kimzuie, hata mbele ya Yesu kujaribu kumkemea, yeye alisema . . . Bali alisimama na kukubali ya kwamba Yeye alisema kweli, Neno lilikuwa sahihi,

na kila kitu. "Lakini hata hivyo, Bwana, mbwa hula makombo, na kombo tu moja kutoka Kwako ndilo ninaloomba. Moja dogo tu moja dogo, chembe moja ndogo ndiyo yote ninayotaka, Bwana. Mguso Wako tu, huo tu ndio ninaotaka. Mguso Wako tu, hivyo tu."

149 Loo, laiti tungalikuwa tu na hiyo usiku wa leo, "Bwana, nimeketi hapa, mimi ni mgonjwa. Lakini kama—kama—kama kitu fulani kitaniambia tu ya kwamba ninaweza kupata nafuu, hilo tu ndilo ninalotaka kujua. Basi hilo—hilo latosha, ninaenda nyumbani na kuliamini, unaona. Hakuna kitu kitakachonizuia tena. Makombo Yako tu, Bwana, ndiyo tu ninayotaka."

150 Yesu akasema, "Ee mwanamke," ama "Ee mwanamke, imani yako ni kubwa. Nenda zako, kwa kuwa yale umeng'ang'ania kuyahusu, yale umeamini, utayakuta jinsi hiyo." Amina.

151 Hatimaye alikuwa ameshinda. Alikuwa na njia nzuri ya kuiendea karama ya Mungu. Alikuwa ni Mmataifa. Imani daima hukubali Neno ni kweli. Kwa unyenyekevu na uchaji, sio kutoka nje na kulipuka kuhusu jambo fulani. Njia ile ile sasa. Upesi sasa, kabla hatujaitisha mstari wa maombi.

152 Martha, mbele za Bwana Yesu, wakati kila mtu alikuwa amemdhihaki, alisema, "Angalia, Jamaa huyu ambaye huwaponya wagonjwa, wakati mlipomhitaji Yeye. . .Naam, mlichukua mali yenu, mkamlisha, mmempa Yeye chumba; wakati Yeye alipokuja jijini, alikaa pamoja nanyi. Alikuwa ni rafiki msiri wa Lazaro. Lakini wakati maradhi yalipoingia kweli, Yeye aliwaacha." Unaona?

153 Lakini aliposikia kwamba alikuwa amekuja, aling'ang'ania. Alitoka akaingia mtaani. Mwingine akasema, "Sasa nadhani unatoka kwenda kumwona Yeye." Yeye aliyafumba tu masikio yake na macho, aliendelea tu kukaza mwendo. Aling'ang'ania.

154 Wakati Yesu aliponena naye, yeye alisema, "Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa. Lakini hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa Wewe." Aling'ang'ania. Angalieni, kama yule mwanamke Mshunami, mbele za Eliya, mwakilishi wa Mungu duniani; Martha alijua, kama Mungu alikuwa ndani ya Eliya, hakika Yeye alikuwa ndani ya Yesu.

155 Mwanamke Mshunami, alipopanda kule juu, na akasema, Elisha alitoka pangoni mwake na kuangalia kule nje na kusema, "Huyu hapa yule Mshunami anakuja, na moyo wake umehuzunika. Mungu amenificha hilo. Sijui anachotaka."

156 Kasema, "Yote ni salama kwako? Mume wako hajambo? Mtoto hajambo?" Akasema, "Wote hawajambo."

157 Mwangalie wakati alipomwambia mtumishi wake. "Tandika nyumbu huyu, kisha uende moja kwa moja mbele wala usisimame." Kung'ang'ania, endelea tu kwenda.

158 Baadhi yao wanasema, "Aisee, simama kidogo! ninataka kuzungumza na wewe, Lydie."

159 "Hakuna kitu, si—sina budi kufika kule, hakuna lingine. Mnaona, sina budi kufika kule. Inanibidi kutafuta kujua kuhusu haya." Halafu basi wakati ninii . . . Akasema, "Vema, nitakwambia, nitakutumia nguo iliyopakwa mafuta. Nitakutumia fimbo hii, nawe nenda kule, ukailaze juu ya mtoto huyo."

160 "Hilo ni zuri sana, nabii wa Mungu. Na—na—nafikiri hilo ni sawa kabisa. Lakini kama nafsi yako iishivyo, sitakuacha, nitakaa papa hapa mpaka nitakapopata kujua." Amina. Kung'ang'ania. Hakika, alikuwa mng'ang'anizi.

161 Eliya akawazia, "Vema, mwondoshe. Afadhali nijifunge viuno vyangu." Mnaona? Huyu hapa akaenda. Mnaona? Kung'ang'ania, imani yao ililishikilia Neno.

162 Jinsi ambavyo maskini Mikaya, maskini yule mtu wa mwituni asiye na elimu kule nyuma, angeweza kusimama mbele ya hao manabii mia nne, na kunena hapo kinyume chao. Kwa nini? Alikuwa mng'ang'anizi.

163 Wao wakasema, "Mbona, angalia!" Yule askofu kiongozi mkubwa mno alisimama pale juu akiwa na hizi pembe, na kusema, "Bwana Mungu alisema nami." Loo, jamani! Kiongozi wa shirika hilo alisema, "Bwana Mungu alisema nami, na ikashuhudiwa na mia nne wa hawa watu hapa, kwamba, BWANA ASEMA HIVI!" Naye mtu huyo alikuwa mwaminifu.

164 Sasa, bali Mikaya akasimama, akasema, "Lakini niliona Israeli wametawanyika, kama kondoo wasio na mchungaji."

165 Kwa hiyo akajongea pale, na kuinua mikono yake na kumpiga kofi mdomoni kwa nguvu alivyoweza, kasema, "Roho wa Mungu alielekea wapi wakati alipotoka kwangu, kama unajua yote kuhusu jambo hili?"

Kasema, "Utaelewa, siku moja." Naye Ahabu akasema . . .

166 Vema, sasa, hivyo ndivyo hilo shirika lilivyosema. Angalieni sasa, kamwe asingeweza kuingia ndani yao wakati huo, chini ya hali kama hizo. Lakini alijua ono lake lilikuwa sahihi. Alikuwa na imani, kwa sababu imani yake ilisema vile vile hasa Neno lilivyosema, kwa hiyo aling'ang'ania.

167 Sasa waangalie watawala wa kitaifa. Hapo alisimama Ahabu, kasema, "Mtieni kwenye gereza la ndani, na mkamlishe mkate na maji ya shida. Ndipo nitakaporudi kwa amani," akasema, "Nita—nitamshughulikia jamaa huyu."

168 Mwangalieni, angali anang'ang'ania. "Loo, Ahabu mkuu, labda nilikosea. Loo, askofu, labda nilikosea"? La, la, sio yeye. Alikuwa ametia nanga. Aliona ono, nalo ono lake liliambatana na Neno. Akasema, "Kama ukirudi kamwe, mimi ni nabii wa uongo!" Amina. Aling'ang'ania. Bila shaka, aling'ang'ania.

169 Yule kipofu niliyenena habari zake muda mfupi uliopita, asingeweza kubishania theolojia pamoja nao, hakujua chochote kuihusu. Wao wangeweza kusema, "Mbona, *Fulani-wa fulani* alisema hivi na hivi na hivi na hivi."

170 Yeye akasema, "Sijui kuhusu theolojia yenu. Bali najua jambo hili moja: ambapo nilikuwa kipofu, sasa naweza kuona."

171 Baba yake na mama kamwe hawakuwa na imani ya namna hiyo. Walisema, "Loo, watatufukuza kwenye sinagogi. Kwa hiyo ninyi mwulizeni, ni mtu mzima."

172 Ndugu, hakuwa na kasoro yoyote. Alisema, "Ni ajabu . . ." Kasema, "Mimi si mwanatheolojia. Siwezi kuyabishania Maandiko yenu mnayozungumzia. Bali mlisema ya kwamba mnajua Mungu aliponya; lakini, Mtu huyu, hamjui alikotoka. Sasa, ni jambo la kushangaza, kwamba Mtu anaweza kuja hapa na anaweza kuyafungua macho yangu mapofu; na nyinyi, viongozi wa dini, na hamjui kule Yeye alikotoka." Ndugu, yeye alikuwa ni mwanatheolojia, katika kitabu changu. A—alikuwa na, alikuwa na hoja isiyotatulika na hao wengine, hivyo tu. "Jinsi ambavyo mnasema hamna taarifa yoyote ya kuja Kwa—Kwa—Kwake, hamna taarifa yoyote kwenye kitabu chenu, ya kisomo Chake, mahali elimu Yake ilikotoka, wala chochote. Hamjui alikotoka, na hata hivyo ndiye Mtu aliyeyafungua macho yangu." Hoja nzuri sana, sivyo? Naam, bwana.

173 Filipo, aliposimama pale na kumwona Yesu wa Nazareti akimwambia Simoni lililokuwa jina lake, na jina la baba yake, aling'ang'ania sana. Alikuwa na rafiki aliyejiona shupavu ambaye alitaka kumwambia habari zake, ndipo akaenda na kumpata Nathanaeli.

174 Wakati Nathanaeli, akisimama pale mbele ya washiriki wa kanisa lake, na kuhani mkuu, na Baraza la wazee, na hao wote wakisimama karibu. Wakati Yesu alipomtazama, na kusema, "Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake."

175 "Loo, afadhali ninyamaze sasa. Kuwa mwangalifu, yule pale amesimama askofu, yule pale amesimama mwangalizi mkuu, yule pale amesimama mchungaji, wale pale jamaa zangu wote wamesimama. Afadhali nitulie, nijifanye tu kana kwamba sijui lolote kulihusu"? Mnaona? La, la.

176 Jambo fulani lilikuwa limetukia. Filipo alikuwa amemwonyesha mbegu. Akasema, "Rabi!"

177 Hao wakisimama pale, wasema, "Mtu huyu ni Beelzebuli. Msisikilize Hilo. Yeye ni mpiga ramli. Yeye ni ibilisi. Msimsikilize Huyo." Lakini Filipo, upesi, ama . . .

178 Nathanaeli alimtambua kama Rabi, mwalimu. Kasema, "Rabi, uliwahi kuniona lini Wewe?"

179 Akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti."

180 "Sasa nitafanya nini? Haya hapa Maandiko, yanasema ya kwamba hiyo ndiyo ishara ya Masihi." Akamwendea mbio na kusujudu, ndipo akasema, "Rabi, Wewe ndiwe Mwana wa Mungu! Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli. Sijali yale wengine wao wanataka kusema juu yake. Wewe ndiwe Mwana wa Mungu, Mfalme wa Israeli."

181 Maskini yule mwanamke kisimani, alipoambiwa shida yake. Sasa, mwajua, kama ikitokea kwamba unajua ninii za Kimashariki . . .

182 Wapo wamishenari hapa, waliowahi kuwa huko Mashariki? Vema, mnafahamu ya kwamba mwanamke kama huyo hana mamlaka yoyote hata kidogo, kuwazungumzia wanaume mahali popote. Hiyo ni kweli. Ingali hivyo. Hazungumzi, hawezi kuwazungumzia wanaume, kwa vyovyote vile, na hasa sana juu ya hoja za kidini na mijadala.

183 Lakini, loo, jamani, ungeweza kumnyamazisha? Ni kama nyu—nyumba kavu iliyoshika moto, katika upepo mkali. Usingeweza kumkomesha. Akasema, "Njoni, mwone Mtu, Yeye aliniambia mambo ambayo nimefanya. Je! haimkini huyu kuwa ndiye Masihi mwenyewe?" Sasa nina . . .

Ninafunga sasa. Sina budi kuondoka.

184 Yapata miaka minne ama mitano iliyopita, niliona ono, kunituma huko Meksiko. Hebu chukueni lile Sauti ya Wafanya Biashara ambalo . . . Mnaona, kabla hujaweza kuchapisha chochote, huna budi kuwa na uwezo wa kukitetea. Sasa, unaweza kukisema, bali usikichapishe isipokuwa unaweza kukitetea, maana ni maandishi. Nilikuwa na . . .

185 Nilishushwa kwa kamba, nyuma ya uwanja wa michezo, kile kizimba tulichokuwamo, tulikuwa na yapata elfu kumi kila usiku, waongofu kwa Kristo. Ndipo basi nilipotazama, Billy alinijia na akasema, "Baba, unaona hayo yote yanayoendelea, kule upande ule mwingine, kama yadi mia moja na hamsini?" Kasema, "Huyo ni maskini mwanamke mmoja." Akasema, "Hana kimo cha kinara cha sabuni, hata, maskini kitu kidogo." Kasema, "Ana mtoto mfu chini ya mkono wake." Kisha kasema . . .

186 Nilimwita mtu huyo *Mañana*, "kesho," alikuwa ni mwenda pole sana, aliyekuja na kunichukua. Alipaswa kunichukua saa moja, naye alinichukua saa tatu. Mimi nikitembea huku na huku sakafuni.

187 Naye alikuwa tayari amesambaza kadi zote za maombi, na hakuwa na zingine. Nilikuwa nimempa tu kama kumi na tano ama ishirini, kila usiku, maana hao tu ndio ningaliweza kuwafikia. Maana, kama ungewapa kadi, ha—hawaelewi kama wewe, huwezi kuwazungumzia. Kwa hiyo walikuwa—walikuwa tu . . . Niliwapa kama kumi ama kumi na tano, chochote kile, hizo tu ndizo ningetoa. Vema, hawakuwa na kadi zingine za maombi.

188 Ndipo kasema, “Hakuingia na mtoto huyo, wala hakupata kadi ya maombi.” Tena kasema, “A-ha, tuna karibu mabawabu mia moja na hamsini, mia mbili, ama labda zaidi, wamesimama pale chini, nao hawawezi kumzuia mwanamke huyo mdogo. Anakimbia chini ya miguu yao, anapanda juu ya migongo yao, na kila kitu kingine. Anaye mtoto huyu aliyekufa.” Alikuwa amemwona huyo kipofu usiku uliotangulia, akifunguliwa macho yake, kwa hiyo akasema alitaka kuingia.

189 Nikasema, kisha nikasema, nikasema, “Billy, si—siwezi kusaidia.” Nilikuwa nikizungumza.

190 Nikasema, “Ndugu Jack Moore,” nikasema, “nenda huko. Yeye hajui mimi ni nani.” Wasingeweza kuniona, huko nyuma kabisa namna hiyo. Basi nikasema, “Nenda kule, kisha ushuke uende ukamwombee mtoto yule, naye atafikiri ni mimi tu, na hilo latosha.”

191 Akasema basi, “Vema, Ndugu Branham.” Akaanza kuelekea kule.

192 Nami nikageuka, nikasema, “Sasa kama nilivyokuwa nikisema, imani ni . . . ” Nikaangalia huko nje mbele zangu, na palikuwa na maskini mtoto mchanga wa Kimeksiko ameketi moja kwa moja katikati ya hewa pale, anacheka tu, kitu kama mtoto mdogo, asiye na meno, wa kunyonya. Ndipo nikaangalia tena.

193 Ndugu Espinoza, wengi wenu mnamfahamu Ndugu Espinoza, “Kwa hiyo kuna nini?”

194 Nikasema, “Ninaona ono.” Nikasema, “Ngoja kidogo, Ndugu Moore.” Nyinyi nyote mnamfahamu Jack Moore, nina hakika, enyi wafanyabiashara. Nikasema, “Ngoja kidogo, Ndugu Moore. Ngoja kidogo. Billy, nenda kamlete mwanamke huyo hapa.”

Kasema, “Baba, hana kadi ya maombi.”

Nikasema, “Haileti tofauti yoyote; mlete hapa.”

195 Basi, yeye, wakampisha. Huyu hapa anakuja maskini mwanamke mrembo kwelikweli, na nanii wake . . . Mvua, inanyesha tu, na imekuwa ikinyesha alasiri yote, nao watu hao wamesimama pale. Nazo nywele za—zake za kupendeza zimening’inia mbavuni mwake, na uso wake, wote umelowa maji. Naye alikuwa akilia, na—na machozi yakitiririka mashavuni mwake. Naye akaja mbio pale juu, amelowa kabisa, na blanketi ndogo iliyoonekana ya samawati imezungushiwa maskini umbo hilo, naye alikuwa amelishikilia namna *hii*. Basi akaanguka magotini mwake na kuanza kusema jambo fulani kwa sauti kuu, “Padre, padre!”

196 Ndipo nikamwangalia, nikasema, “Simama.” Ndugu Espinoza akamwambia. Naye alikuwa na maskini mtoto huyo mchanga namna *hiyo,* amemshika, kama tu vile ningeishika leso

hiyo, ila tu alikuwa amelala kuikingama mikono yake namna *hii*.

197 Nami nikasema, “Baba wa Mbinguni, sijui kama huyu ndiye yule mtoto mchanga ama siye. Nilimwona tu maskini mtoto mchanga, na nafikiri labda huyu alikuwa ndiye, kwa kuwa hili limetukia jinsi lilivyotukia. Na—naweka mikono yangu juu yake na kuomba ili uhai urudi, katika Jina la Bwana Yesu.” Ndipo maskini mtoto huyo akarusha teke, na kuanza kupiga mayowe kwa nguvu alivyoweza. Mnaona?

198 Nami nikasema, “Ndugu Espinoza, usiseme lolote juu ya hilo sasa. Usiwape hilo wafanyabiashara, au yeyote wao, mpaka utakapopata taarifa iliyotiwa sahihi kutoka kwa daktari wake.”

199 Basi daktari akatia sahihi taarifa hii, kwamba, “mtoto huyo mchanga alikufa kwa nimonia” ofisini mwake “asubuhi hiyo saa tatu,” na hii ilikuwa karibu sana na saa tano usiku, alikuwa mfu wakati huo wote.

200 Kwa nini? Aling’ang’ania. Aliamini, kama Mungu angeweza kuyafungua macho ya kipofu. . .Utukufu kwa Mungu! Kama Mungu anaweza kumfanya kipofu aweze kuona, Mungu angeweza kumpa uhai mtoto huyo mchanga; maana Mungu yeye yule aliyemfungua macho kipofu, atampa uhai mtoto huyo mchanga. Kwa nini? Aling’ang’ania. Mabawabu mia tatu, hakuna kitu kingaliweza kumkomesha. Aliyakinia, maana kitu fulani kilitia nanga.

201 Kamwe hakuwa ameona lolote la mambo haya mnayoyaona nyinyi nyote. Jambo pekee, mtu fulani alimwambia, siku hiyo, kwamba mtu kipofu, aliyeishi chini ya barabara kutoka mahali yeye alipokuwa, alikuwa amefunguliwa macho yake; alikuwa kipofu kwa karibu miaka kumi, akiwa na glakoma katika macho yake. Na siku hiyo, alikuwa akitembea mtaani, akilia, akiitikisa mikono yake, naye mama huyo akamwona.

202 Basi mtoto wake mchanga akafa. Akamchukua mtoto huyo mchanga kutoka ofisini mwa daktari, na kuondoka. Akasimama kwenye mvua hiyo siku nzima, akiingojea nafasi yake. Na wakati hakupata kadi ya maombi, angali aling’ang’ania. Hakujua chochote; alikuwa ni Mkatoliki wa Kirumi. Jambo pekee alilojua, ni kwamba ilimbidi kumfikia mtu fulani.

203 Sasa ninyi mnajua vyema zaidi ya hilo. Si mtu unayemwendea. Ni Kristo ndiye unayemwendea. Ni Bwana Yesu Kristo ndiye unayemwendea. Imani yake yote ilikuwa katika kuhani wake, kwa sababu alikuwa ni mungu kwake. Lakini usiku wa leo hakuna mtu aliye mungu wako ila Yesu Kristo, na Yeye yupo hapa, yeye yule jana, leo, na hata milele. Haleluya!

Hebu tuwe wang’ang’anizi, tunapoinamisha vichwa vyetu.

204 Bwana Yesu, ninaomba ya kwamba Wewe utusaidie sasa. Neno moja tu ama mawili kutoka Kwako, Bwana, yanapaswa tu kufanya jambo fulani kwa watu hawa. Ninakuomba Wewe, Bwana. Kama Wewe ulivyoahidi katika siku za mwisho ya kwamba Wewe ungefanya mambo haya, kazi ulizofanya Wewe ulipokuwa hapa duniani, ambazo zingerudiwa tena, na ukatoa mifano yake kote katika Maandiko; kama vile, kwa mfano, Sodoma na mahali mbalimbali, nasi tunaona humu katika Kitabu cha Ufunuo, katika Wakati wa Laodikia. Na, loo, jinsi ambavyo Wewe ulifanya ahadi, na kusema Wewe ulikuwa ni "yeye yule jana, leo, na hata milele"! Nasi tunaliona kwa picha, wakati jicho la kimitambo la kamera litashika siri katika siku hizi za mwisho, ambazo mwanadamu hawezi kueleza. Mungu, wajalie wanaume na wanawake, usiku wa leo, wanaoteseka na ni wagonjwa, hapa, jalia wang'ang'anie na wamfikie Bwana Yesu katika saa hii, waende nyumbani wakishangilia, wameponywa. Tunaomba hayo katika Jina Lake, kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

205 Sasa, ningali nimechelewa. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Lakini ninafikiria hili, "Huenda huu ukawa ndio mkutano wa mwisho tunaofanya pamoja. Huenda nisiwaone tena. Huenda msinione tena mpaka tutakapouvuka ule mto." Na sisi sote huenda tukavuka kabla ya asubuhi.

206 Kumbukeni, taifa hili limepimwa katika mizani. Tutalifikia hilo nitakapoanza kuhubiri, mnaona. Angalieni, hatujui itakuwa lini.

207 Kwa hiyo, Paulo alihubiri usiku kucha, usiku mmoja, Injili ii hii. Bwana aliliheshimu Neno Lake, wakati jamaa mdogo alipoanguka akafa, kama vile Ndugu Way alivyofanya majuzi asubuhi. Ameketi papa hapa mbele zangu sasa. Paulo aliulaza mwili wake juu ya mvulana huyu, ndipo uhai wake ukamrudia. Hilo ni jambo lile lile lililomfanyia Ndugu Way. Inaonyesha ya kwamba Mungu yule yule, kwa Neno lile lile, kwa Roho yule yule, hufanya jambo lile lile. Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Basi ikiwa Yeye yupo hapa . . .

208 Sasa angalieni, hakuna mtu awezaye kukuponya, maana tayari umeponywa. Jambo fulani halina budi kutukia ndani yako, kukwambia ya kwamba ni kwa ajili yako, kisha ung'ang'anie.

209 Hebu tuone, hizo kadi tulizosambaza zilikuwa zipi, zilikuwa za A, A? Loo, ndio kwanza umalize kusambaza hizo zingine za A? Vema. Tulianzia wapi? Na za moja, zi- . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Tulianzia, tulikuwa na kumi na tano, ninaamini ndivyo ilivyokuwa, moja hadi kumi na tano, moja hadi kumi na tano.

210 Hebu tuanzie mahali pengine hapo, na hebu tuanzie kutoka sabini na tano, themanini, tisini. Hebu twende kwa tisini, sabini

na tano hadi tisini. Tuchukue kundi dogo mle ndani, na kuanzia pale, halafu tupate wakati tukiendelea kutoka hapo. Tuanzie tu kutoka pale. Tuone kama tunaweza kupata wengi tuwezao, kuwaombea. Hebu kadi za maombi sabini na tano hadi tisini, wasimame kwanza. Hiyo itatupatia kumi na watano wa kuanzia. Tutaona vile Roho Mtakatifu atakavyoongoza. Waleteni hapa upande wa kulia, tafadhalini, kumi na tano hadi tisini . . .

211 Ama ngojeni, samahani. Nilisema nini? [Ndugu Vayle anasema, "Sabini na tano hadi tisini."—Mh.] Sabini na tano hadi tisini. ["Watu kumi na sita."] Watakuwa ni kumi na sita, naam, sabini na tano hadi tisini. Hao watakuwa ni watu kumi na sita. Vema, wewe nisaide, Ndugu Vayle. Sasa ikiwa . . . ["Wanakuja."] Wako pale. Kama hawawezi kusimama, mbona, uhakikishe kwamba watapata usaidizi hapo chini. Vema, Ndugu Vayle, tafadhali. Sasa nataka . . .

212 Ni wangapi hapa ndani ambao hawana kadi za maombi, nanyi mnataka, unajua ya kwamba Yesu Kristo anaweza kukuponya, inua mkono wako, useme, "Na—nataka kuukubali. Ni—ninaamini." [Ndugu Branham anatulia—Mh.] Loo, haitatulazimu kumngojea Roho Wake, tayari nimemwona Yeye akimgusa mtu fulani pale pale kwenye kusanyiko. Amina.

213 [Ndugu Vayle anasema, "Wanne hawako."—Mh.] Kadi nne hazipo, kati ya sabini na tano na tisini. ["Wanaingia ndani sasa."] Vema.

214 Ni wangapi huko nje, ni wangapi huko upande wa nyuma kabisa, wanaamini, nyuma kabisa upande wa nyuma, huko juu kabisa kwenye roshani, kote? Sema tu, "Ninaamini." Inua mkono wako, useme, "Ninaamini." Vema, jambo ndilo hilo. Hilo ni jema. Sasa kama Yesu Kristo . . .

215 Wakati nikiwazia hapa, ninangojea kuona kama kweli itafanya kazi juu ya mtu huyu, ama haitafanya. Mtu fulani aliguswa wakati uo huo tu. Nililiona likitukia. Sijawahi kumwona mtu huyo maishani mwangu. Lakini niliwaangalia moja kwa moja, nikaliona likitukia, na nikamwona mtu huyo akiguswa na Roho Mtakatifu. Ningeweza kumfanya mtu huyo asimame moja kwa moja sasa, na kuthibitisha kwamba ni kweli, amina, kabla mstari haujapata kuanza. Angali anaomba, ameweka leso yake kinywani mwake, ameketi moja kwa moja kule nyuma. Ana shida ya uti wa mgongo. Hiyo ni kweli. Unayeketi moja kwa moja . . . Naam. Huyo ni mume wako, aliyeinua mkono wake. Sikiliza, mimi ni mgeni kwenu nyote, hiyo ni kweli? Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Shida yako ya uti wa mgongo itakuacha.

216 Pia sikiza, jambo jingine, yule mwanamume aliyeinua mkono wake, kwa kuwa Roho Mtakatifu alikugusa; nilipozungumza na mke wako, Roho Mtakatifu alikugusa. Nawe

una shida fulani, uvimbe mkononi. Amini, nao utakuacha. Utukufu kwa Mungu!

217 Waulizeni hao watu kama niliwahi kuwaona maishani mwangu, nijuavyo mimi. Hao ni wageni. Lakini nini? Imani ikitenda kazi, na nguvu za Roho Mtakatifu. Je! mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Amina.

218 Unazungumza Kihispaniola? Geuka na umwambie maskini msichana yule, hawezi kuzungumza Kihispaniola...hawezi kuzungumza Kiingereza, huko nyuma. Ana shida fulani kifuani mwake. Geuka ukamwambie. Yesu Kristo alikuponya, dada. A-ha. Naam. Hata asingeweza kuzungumza Kiingereza. Nilimwona akizungumza Kihispaniola.

219 Sasa Hiyo imemwendea mama mwingine, aliyeketi mbele yake, amesisimkwa kwelikweli, naye hawezi kuzungumza Kiingereza. Yeye ni Mhispaniola, naye ana shida fulani tumboni mwake, aliyeketi hapo mbele. Amini kwa moyo wako wote, shida yako ya tumbo inakuacha, nawe unaweza kwenda nyumbani na uwe mzima. Amina. Mungu ndiye Mponya.

220 Mnaiona Hiyo ikimgusa? Iliwabidi kumwambia, katika Kihispaniola, kabla yeye hajatambua. Hawezi kuelewa Kiingereza. Angalieni pale, watu ambao hata hawawezi kuzungumza Kiingereza! Ila kile tu wanachoona, wao—wanaweza kudhania na kuhisi Roho, hata wakati ambapo hawawezi hata kusikia.

Aibu kwenu!

221 Utukufu kwa Mungu! Sijawahi kuona hilo likitendeka bado. Amina. Waulizeni hao watu. Mbona, hata siwezi kuzungumza lugha yao. Lakini, mnaona, inathibitisha si lazima uwe kwenye mstari huu wa maombi. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaamini?

222 Kwa nini ukasema "amina," unayeketi papo hapo? Unaamini shida hiyo ya pua itakuacha? Unaamini? Simama kwa miguu yako. Inakuacha.

223 Unaona, anaweza kunisikia, yale ninayosema; *hawa* wasingeweza. Sasa mniambie ati si Mungu? Amina na amina. Kwa nini msing'ang'anie, kama hao watu wasioweza kuelewa neno, neno moja la Kiingereza, wanajitahidi kuingia? Walikuwa ni wa taifa jingine. Lakini Mungu alifanya jambo hilo, ninaamini, kwa sababu nilihubiri hivyo dakika chache zilizopita, "Myunani, taifa jingine." Aling'ang'ania. Waangalieni, muone linalotukia.

224 Je! huyu hapa ndiye huyo mama? U hali gani? Hatufahamiani sisi kwa sisi. Unaamini Yesu Kristo yupo? Kukuponya, nisingeweza. Sina ngu—nguvu za kuponya. Ninayo mamlaka wakati nikiyapokea kutoka kwa Mungu, kutangaza jambo fulani ambalo Mungu amefanya. Mnaona?

225 Na kama vile Samsoni, mradi tu angeweza kuhisi vishungi hivyo vikining'inia hapo, ilikuwa ni sawa. Ninapomwona Yeye akitenda kazi miongoni mwetu namna hii, ninajua Yeye yupo hapa. Nanyi je? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

226 Ninakuona ukitapika. Una vipindi vya kutapika. Unahangaika juu ya uzito wako uliozidi. Tena, una uvimbe mwilini mwako, chini ya ubavu wako. Hiyo ni kweli. Ulikuwa na wakati mgumu sana kupanda kuja hapa, sivyo? Ni kwa nini nikasema, "Panda huku juu"? Kwa sababu umekuja kutoka—kutoka kusini-magharibi kutoka hapa. Umetoka Missouri. [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Rudi, Yesu Kristo anakuponya. Huyo ni Yeye.

227 Mwanamke mwingine, mwanamke mweusi, simjui, sijawahi kumwona. Lakini yeye ni. . .Kuna mtu anayekuja hapa, mwingine, jamii nyingine ikikutana mmoja na mwingine, ya mzungu na ya mtu mweusi. Sisi sote ni wa damu moja. Unaamini Mwana wa Mungu alifufuka kutoka kwa wafu, na Yeye aliliagiza kanisa Lake kufanya jambo lile lile alilofanya Yeye? Unaamini hilo? Kanisa hilo haliwezi kufa. "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, malango ya kuzimu hayawezi kushinda." Ilikuwa ni kitu gani? Ufunuo wa kiroho. Kama Mungu anaweza kunifunulia, kwa Roho Wake, kusimama kwako hapa, na shida uliyo nayo, jinsi tu Yeye alivyomwambia yule mwanamke kisimani, hilo linamfanya Yeye yule, kwa sababu wewe ni. . .sote wawili ni wanadamu. Hiyo ni kweli?

228 Sasa una wasiwasi sana kuhusu jambo fulani. Una wasiwasi. Akili yako imevurugika sana. Umeambiwa jambo fulani ambalo limekushtua, hilo lilikuwa kwamba una uvimbe, na uvimbe huo uko kichwani mwako. Hiyo ni kweli. Na wewe—umepangiwa upasuaji, bali kidogo wanahofia jambo hilo, kwa sababu una udhaifu moyoni mwako, kwamba wanahofia kufanya huo upasuaji kwa sababu ya udhaifu wa moyo wako. Yesu Kristo anautia nguvu moyo wako. Unamwamini Yeye? Anaweza kuuponya uvimbe wako. Unamwamini Yeye? Basi ng'ang'ania. Endelea, endelea. Nenda ukaamini, utapona. Mungu akubariki.

229 U hali gani? Mwanamume mwingine, simjui. Nilimwona muda mfupi uliopita, nilipokuja jukwaani, ninaamini alikuwa ameketi hapa juu. Mara ya kwanza niliyopata kukuona maishani mwangu, nijuavyo mimi. Vema. Sasa upo hapa kwa sababu fulani. Kama mimi pamoja na Roho huyu aliye juu yangu, ile Nguzo ya Moto na Nuru, na kadhalika, iliyopigwa picha, kama hiyo ni ya Yesu Kristo, Hiyo italishuhudia Neno; isipolishuhudia, basi si ya Kristo. [Huyo ndugu anasema, "Kweli."—Mh.] Lakini umeshawishika kwamba ndiyo. ["Naam."] Nawe umeshawishika. Na wewe unaugua ugonjwa wa wasiwasi, bawasiri inayokusumbua. Na unajaribu upate kuniona ["Naam."] juu ya jambo fulani maalum. ["Naam."] Ni shida ya

kiroho. ["Naam."] Wewe ni mhudumu. ["Naam. Naam."] Na ni kuhusu kanisa lako. ["Naam."]

230 Nilisikia hilo likitoka kwako. Achana na wewe kuwazia hayo. "Unasema alikuwa ni mhudumu kwa sababu alikuwa ameketi kwenye jukwaa hili."

231 Unajua sikujui, sivyo? [Ndugu huyo anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? ["Naam. Amina. Ninaamini."] Basi, Kasisi Donaldson, unaweza kurudi nyumbani kwako, na uamini, nawe utapata afya na kila kitu kitakuwa sawa kwako. Mungu akubariki, mchungaji.

"Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana."

232 Unaamini? Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? [Dada huyo anasema, "Amina."—Mh.] Unajua kwamba siwezi kufanya mambo haya? ["Hiyo ni kweli. Utukufu!"] Lakini unaamini ya kwamba Yeye anayafanya, Yeye ndiye anayeyafanya? ["Hiyo ni kweli."] Unaamini hilo?

233 Hiyo ni sawa, kama utaninii tu—sasa hivi tu kwa wakati huu mmoja tu, naomba, shikilieni, msiruhusu chochote kiwazuie. Jitahidini kuingia. Hivi hamwoni ni Yeye? Hamjui huyo ni Yeye? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

234 Mnaona, Yeye asingejitambulisha Mwenyewe kama mwanatheolojia mkuu, ambaye Yeye hakuwa hivyo. Asingejitambulisha Mwenyewe kama mwa—mwanasiasa wa kanisa, Yeye hakuwa hivyo. Alikuwa ni Mungu, aliyefanyika mwili. Mungu ni Neno, nalo Neno ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Hivi hamwezi kuona kwamba ni Yeye? Ningewezaje mimi, maskini mtu asiye na elimu, kama mimi, nikiwa na elimu ya msingi? Na haijalishi kama ningalikuwa na elimu nyingi, bado usingeweza kufanya jambo hilo. Ni kitendawili. Ni kitu gani? Ni nguvu za Mungu. Hivi hamwezi kuona, enyi marafiki? Je! unaweza kuvunja ganda hilo likuondokee?

235 Huyu hapa mwanamke. Angalia hapa. Sijawahi kumwona mwanamke huyo. Hii hapa Biblia imewekwa mbele yangu, sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu, kadiri nijuavyo mimi. Lakini, maisha yake, asingeweza kuyaficha. Kweli. [Huyo dada anasema, "Loo, haleluya!"—Mh.] Amina. ["Haleluya!"] Sasa, si kwa sababu anasema "haleluya," wanafiki wanaweza kusema hivyo, lakini mwanamke huyu ni Mkristo. Yeye ni mwaminio. ["Loo, haleluya!"]

236 Na kama nitakwambia, kwa neema ya Mungu, nikivihisi vile vishungi saba vya Samsoni, kile ambacho ni shida yako, utaniamini mimi? Kusanyiko litaamini? Kila mmoja wenu ataamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."] Yeye atajua kama ni kweli ama si kweli.

237 Jambo la kwanza, unaugua ugonjwa wa shinikizo kuu la damu. Pia una kisukari. Una ugonjwa wa wasiwasi, na una shida fulani kichwani. Ni kupimwa. Una uvimbe, hiyo ni hakika, kichwani. Nawe unajua ni mauti isipokuwa Mungu akuguse, ama kitu fulani. Hiyo ni kweli? Mungu wa Mbinguni, Yule aliyesimama hapa sasa…Njoo hapa, hebu niweke mikono yangu juu yako. "Ninamlaani ibilisi huyu. Katika Jina la Yesu Kristo, na aondoke." Mungu akubariki. Nenda zako, ukishangilia sasa. Amina.

238 Unaamini? Unasema, "Ulikuwa ukimwangalia moja kwa moja usoni." Si lazima umwangalie usoni pake. Angalieni hapa, sijamwangalia mwanamke *huyu* usoni. Sasa unasema, "Yeye ni mnene." Hiyo ni kweli. "Ni kikoromeo." Hiyo ni kweli. Lakini hilo silo, hilo silo analotaka maombi kwa ajili yake.

239 Anayo shida ya kike, mtoko wa uchafu anaotaka uombewe. Hiyo ni kweli, mama? [Dada huyo anasema, "Ndiyo. Haleluya!"—Mh.] Umekuacha sasa. Nenda zako, huku ukishangilia, ukisema, "Asante, Bwana."

Amini tu.

240 Anemia. Unaamini kwamba Mungu anaweza kukuponya? Sema, "Asante, Mpendwa Yesu." Nenda zako moja kwa moja, ukisema, "Mungu asifiwe," na uamini.

241 Unaonekana mzuri na mwenye nguvu. Unaamini Mungu anaweza kuponya ugonjwa wa tumbo, akupe afya? Nenda, ukale. Yesu Kristo atakuponya.

242 Kristo asipokugusa, huna budi kufa, nawe unajua hilo. Naam, bwana. Lakini Mungu anaweza kuchukua kila ibilisi wa kansa, Yeye anaweza kukiua kitu hicho, na kuuponya. Unaamini? [Dada huyo anasema, "Ninaamini."—Mh.] Nenda, amini. Katika Jina la Yesu Kristo, unaweza kwenda ukaponywe.

243 Hutembei kama unayo, kwa wakati huu tu, bali una yabisi kavu. Pia una mguso wa ugonjwa wa moyo, kusongwa kidogo kwenye moyo. Yesu Kristo anakuponya, kama ukiamini. Unaamini? Ukishangilia, ukisema, "Asante, Bwana," na uponywe.

244 Unaamini Mungu anaweza kuponya mgongo wako na kukupa afya? [Dada huyo anasema, "Amina."—Mh.] Vema, nenda zako moja kwa moja, ukisema, "Asante, Bwana Yesu." Naam. Hiyo ni kweli.

245 Unaamini Mungu anaweza kuuchukua huo, akufanyie ubadilishaji wa damu, na kuondoa hiyo sukari na kukufanya mtu mpya kabisa? Unaamini hilo? Ubarikiwe. Nenda zako, ukishangilia, ukisema, "Asante, Bwana. Ninaamini."

246 Unaamini Mungu anaweza kuondoa uvimbe huo na kukupa afya? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Nenda moja kwa moja, shangilia.

247 Mungu anaweza kuponya baridi yabisi yako na kukunyosha tena, akupe afya. Unaamini hilo? Nenda zako, ukishangilia, na uamini.

248 Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Sikujui; Mungu anakujua. Wewe ni mgonjwa, wewe mwenyewe. Lakini unachotaka sana ni mtu mwingine, watu wawili wagonjwa, wagonjwa sana, kansa, wanakufa. Amini kwa moyo wako wote. *Zichukue*, iweke juu yake, amini na usitie shaka. Watapata afya, kama utaamini. Kuwa na imani.

249 Vema, bwana. Ninaamini wewe ni mmoja wa wahudumu walioketi hapa jukwaani. Kuhusu kukujua wewe, sikujui. Yesu Kristo anaujua moyo wako. Anajua kilicho ndani ya mwanadamu. Unaamini hilo? [Ndugu huyo anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Kama Mungu ataniambia kilicho shida yako, basi uko tayari? ["Naam."] Uko tayari.

250 Ninyi wahudumu mnamfahamu mtu huyu, naamini? [Mtu fulani anasema, "Ndugu Turner."—Mh.] Naam. Vema, mnamjua.

251 Vema, jambo ni kwamba, kwamba wewe kweli, shida ni, unaugua ugonjwa wa kurukwa na akili. Una namna fulani ya mhangaiko wa akili niani mwako. Ni dhuluma kutoka kwa Shetani. Hii imekuwa ikiendelea kwa muda fulani. Imesasabisha mwili wako kudhoofika. Moyo wako ni dhaifu. Uko katika hali mbaya sana. Kwa jambo hili, familia yako yote karibu wameingia katika hali ya kuvurugika. Bwana, umekuwa ukingojea neno, sivyo? [Ndugu huyo anasema, "Naam."—Mh.] Je! unalikubali neno langu? ["Naam, bwana."] Basi, katika Jina la Yesu Kristo, ninakutuma nyumbani uwe mzima. Ibilisi huyo ametoka!

252 [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Mnaamini? ["Amen."] Mnaamini? ["Amina."]

253 Sasa wekeaneni mikono mmoja juu ya mwingine. Sasa nawatakeni muombe pamoja nami.

254 Bwana Yesu, Uwepo Wako mkuu wa Kiungu, hakuna mtu angaliweza kutilia shaka. Kila mtu anajua ya kwamba Wewe upo hapa. Lakini wanajua ya kwamba ni Wewe, sasa acha wang'ang'anie. Wajalie hawa, Bwana, ambao. . . Miujiza hii, wamejaa kwenye mstari mzima, kumi na sita hapa mstarini, na kundi moja huko nje katika kusanyiko, juu ya chochote ambacho mwanadamu yeyote duniani angeweza kufanya, mwenyewe. Hakuna mtu wa duniani hapa angeweza kufanya mambo haya Mungu asipokuweko. Tunajua hilo. Jinsi ilivyo kamilifu, jinsi ilivyo sahihi! Ninakuomba Wewe, Baba, kuwaruhusu watu waone hili, na jalia wawe wang'ang'anizi sasa. Wamewekeana mikono mmoja juu ya mwingine, na mioyoni mwao inapiga, sana, Damu ya kifalme ya Yesu Kristo, kwa imani, wakivuta kila mmoja kutoka kwa mwenzake.

255 Na sasa, Bwana, yasikie maombi ya mtumishi Wako. Kama mtumishi Wako, ninalaani kila maradhi, kila ugonjwa ulio katika Uwepo wa Kiungu wa Kristo aliyefufuka. Naomba ibilisi apoteze mshiko wake. Jalia kila askari, sasa huku upanga wake umeshikamanishwa dhidi ya shaka la Shetani, pamoja na imani ng'ang'anizi, asimame, akiusukuma huo upanga mpaka uchome sehemu ya ndani kabisa ya huyo ibilisi na kumfukuzia mbali kabisa. Tujalie, katika Jina la Yesu Kristo.

256 Kama mtaliamini, kama mkilikubali, nyote mmeponywa. Liaminini, katika Jina la Yesu Kristo.

63-0802 Mng'ang'anizi
Marigold Center
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org